# HOTUBA YA WIZARA YA NISHATI NA MADINI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

## ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA KATIKA HOTUBA YA MWAKA 2017/18

| | |
|---|---|
| AFD | Agence Française de Développement (French Agency for Development) |
| AfDB | African Development Bank |
| AFG | Arusha Germ Fair |
| BADEA | Bank of Arab for Economic Development in Africa |
| BOO | Build Own and Operate |
| BOOT | Build Own, Operate and Transfer |
| BTIP | Backbone Transmission Investment Project |
| CAMARTEC | Centre for Agriculture Mechanization and Rural Technology |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| CDA | Capital Development Authority |
| CHADEMA | Chama cha Demokrasia na Maendeleo |
| CIDA | Canadian International Development Agency |
| CIF | Climate Investment Fund |
| CNOOC | China National Offshore Oil Company |

| | |
|---|---|
| DBSA | Development Bank of Southern Africa |
| DfID | Department for International Development |
| Dkt | Daktari |
| DSE | Dar es Salaam Stock Exchange |
| EDCF | Economic Development Cooperation Fund |
| EIPC | Electricity Infrastucture Procurement Coordinator |
| EPP | Environmental Protection Plan |
| EU | European Union |
| EWURA | Energy and Water Utilities Regulatory Authority |
| FEED | Front End Engineering Design |
| GIZ | Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit |
| GNT | Government Negotiation Team |
| GRMF | Geothermal Risk Mitigation Fund |
| GST | Geological Survey of Tanzania |
| GWh | Gigawatt Hour |
| HGA | Host Government Agreement |
| ICEIDA | Icelandic International Development Agency |

| | |
|---|---|
| ICGLR | International Conference on Great Lakes Region |
| IDA | International Development Association |
| IGA | Inter-Governmental Agreement |
| IOCs | International Oil Companies |
| IPP | Independent Power Producers |
| JBIC | Japan Bank for International Cooperation |
| JICA | Japan International Corporation Agency |
| KfW | Kreditanstalt für Wiederaufbau |
| KPCS | Kimberly Process Certificate System |
| kV | Kilovolt |
| LNG | Liquefied Natural Gas |
| LPG | Liquefied Petroleum Gas |
| Mb | Mbunge |
| MDAs | Mining Development Agreements |
| Mhe | Mheshimiwa |
| MoU | Memorandum of Understanding |
| MRI | Mineral Resource Institute |
| MW | Megawatt |
| NACTE | National Council for Technical Education |

| | |
|---|---|
| NBS | National Bureau of Statistics |
| NDC | National Development Corporation |
| NDF | Nordic Development Fund |
| NGUMP | Natural Gas Utilization Master Plan |
| OC | Other Charges |
| OFID | OPEC Fund for International Development |
| OMCTP | Online Mining Cadastre Transactional Portal |
| ORIO | Infrastructure Development Facility (Ontwikkelingsrelevante Infrastructuurontwikkeling) |
| PBPA | Petroleum Bulk Procurement Agency |
| PE | Personal Emolument |
| PPP | Public Private Partnership |
| PPRA | Public Procurement Regulatory Authority |
| PSMP | Power Sytem Master Plan |
| QDS | Quarter Degree Sheet |
| REA | Rural Energy Agency |
| REE | Rare Earth Elements |
| SCADA | Supervisory Control And Data Acquisition |

| | |
|---|---|
| SE4ALL | Sustainable Energy for All |
| Sida | Swedish International Development Cooperation Agency |
| SMMRP | Sustainable Management of Mineral Resources Project |
| SPM | Single Point of Mooring |
| SREP | Scaling-Up Renewable Energy Program |
| SSMP | Sustainable Solar Market Packages |
| STAMICO | State Mining Corporation |
| TAKUKURU | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| TANESCO | Tanzania Electric Supply Company Limited |
| TANSORT | Tanzania Diamond Sorting Unit |
| TAZAMA | Tanzania - Zambia Pipeline Limited |
| TCF | Trillion Cubic Feet |
| TEDAP | Tanzania Energy Development and Access Expansion Project |
| TEITI | Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative |
| TGC | Tanzania Gemological Centre |
| TGDC | Tanzania Geothermal |

| | |
|---|---|
| | Development Company Limited |
| TIB | Tanzania Investment Bank |
| TMAA | Tanzania Minerals Audit Agency |
| TML | TanzaniteOne Mining Limited |
| TPA | Tanzania Ports Authority |
| TPC | Tanganyika Planting Company Limited |
| TPDC | Tanzania Petroleum Development Corporation |
| TRA | Tanzania Revenue Authority |
| UKIMWI | Ukosefu wa Kinga Mwilini |
| UNDP | United Nations Development Programme |
| UNEP | United Nations Environment Programme |
| USAID | United States Agency for International Development |
| VVU | Virusi vya UKIMWI |
| WB | World Bank |
| WDL | Williamson Diamonds Limited |

## HOTUBA YA WIZARA YA NISHATI NA MADINI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### A. UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha mpango na makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema sisi Waheshimiwa Wabunge wote na hivyo kutuwezesha kuendelea na utekelezaji wa majukumu yetu ya kitaifa ndani na nje ya Bunge. Kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu, Bunge limeendelea kutekeleza majukumu yake ya kikatiba likiwemo la kusimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

*Chanzo: BEA, 2017*

3. ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii kuwapongeza kwa dhati viongozi wetu wa kitaifa kwa jinsi wanavyojituma katika kutatua matatizo na changamoto mbalimbali za Taifa letu na hatimaye kuwaletea wananchi maendeleo. Viongozi hao wameendelea kutoa miongozo ambayo kila mara imekuwa ikilenga kuwaondolea wananchi kero mbalimbali katika maeneo yao. Dhamira hii imedhihirika wazi kwa jinsi Serikali ya Awamu ya Tano inavyoshughulikia masuala yenye maslahi ya kitaifa yakiwemo ya vita dhidi ya rushwa, madawa ya kulevya, ubadhirifu wa mali za Umma, malipo hewa pamoja na kurudisha uwajibikaji Serikalini.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali yake jinsi anavyochukua hatua za kusimamia na kulinda rasilimali za Taifa hasa madini.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba

*Chanzo: REA 2017*

pia kumpongeza Makamu wa Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kazi yake nzuri anayoendelea kuifanya tangu alipoteuliwa. Aidha, nampongeza Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) kwa jinsi anavyoendelea kusimamia kwa karibu shughuli za Serikali tangu Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani. Ni wazi kuwa Viongozi wetu hao wa kitaifa kwa kipindi kifupi walichokaa madarakani wamefanya kazi nzuri na kubwa kwa kutoa na kutekeleza miongozo makini ya kulisaidia Taifa letu. Tuwaombee wote kwa Mwenyezi Mungu ili waendelee na kasi hiyo ambayo imekuwa ni chachu ya mabadiliko katika nyanja mbalimbali na hatimaye nchi yetu iweze kupiga hatua za kimaendeleo kwa kasi kubwa zaidi.

**6. *Mheshimiwa Spika,*** nikupongeze wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Wenyeviti wote wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge lako Tukufu pamoja na Watendaji wa Ofisi ya Bunge kwa jinsi mnavyoliendesha Bunge letu Tukufu kwa ufanisi mkubwa. Nitoe Shukrani za kipekee pia kwa Mhe.

Doto Mashaka Biteko (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Mhe. Deogratias Francis Ngalawa (Mb.), Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Aidha, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. Kwa kweli, nikiri kuwa Kamati hii imekuwa msaada mkubwa katika usimamizi na uendelezaji wa Sekta za Nishati na Madini nchini kutokana na maoni na ushauri wao wanaoutoa kwa Serikali kupitia Wizara yangu.

**7. *Mheshimiwa Spika,*** naomba kuungana pia na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya walioteuliwa hivi karibuni na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ni: Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete; Mheshimiwa Abdallah Majura Bulembo; Mheshimiwa Anne Killango Malecela; na Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Rwakatare, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Viti Maalum kupitia CCM.

*Chanzo: REA 2017*

Pia, nampongeza Mheshimiwa Juma Ali Juma, Mbunge wa Jimbo la Dimani kwa heshima kubwa aliyopewa na wananchi wa Jimbo la Dimani ili awawakilishe kwenye Bunge hili la kumi na moja (11). Vilevile, nimpongeze Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Viti Maalum kupitia CHADEMA. Niwapongeze pia Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kuiwakilisha nchi yetu katika Bunge la Afrika Mashariki na ni matarajio yetu kuwa Wabunge hao wenzetu watatuwakilisha kwa ufanisi na umakini mkubwa kwenye Bunge la Afrika Mashariki.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** nikupe pole wewe binafsi na Bunge lako Tukufu kwa kumpoteza mwenzetu tuliyekaa naye humu kwa muda mrefu, marehemu Samwel Sitta aliyekuwa Mbunge Mstaafu wa Jimbo la Urambo Magharibi, Spika Mstaafu wa Bunge la Tisa (2005 – 2010) na Mwenyekiti wa Bunge la Katiba. Wote tunakiri kuwa Kiongozi huyo alikuwa mchapakazi, hodari na mwenye msimamo katika masuala yenye tija kwa Taifa. Vilevile, nitoe pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuwapoteza Mheshimiwa

*Chanzo: REA, 2017*

Hafidh Ali Tahir, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani, Zanzibar; pamoja na Mheshimiwa Dkt. Elly Marko Macha, Mbunge wa Viti Maalum wa CHADEMA. Naungana na Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia za marehemu. Pia, natoa pole nyingi kwa wazazi, walezi, ndugu na familia za wanafunzi wa Shule ya Msingi Lucky Vicent waliopoteza maisha katika ajali ya gari iliyotokea Wilayani Karatu hivi karibuni. Msiba ni suala gumu, lakini hatuna la kufanya zaidi ya kumwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amen.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo ya awali, naomba sasa kuwasilisha **Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 pamoja na Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18**.

*Chanzo: REA, 2017*

## B. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA WIZARA YA NISHATI NA MADINI KWA MWAKA 2016/17 PAMOJA NA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2017/18

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** Maeneo ya Kipaumbele kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 katika Sekta ya Nishati ni pamoja na: kuimarisha uzalishaji, usafirishaji na kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme nchini; Kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Sekta Ndogo ya Umeme *(Electricity Supply Industry Reform Strategy and Roadmap)*; Kuendeleza Nishati Jadidifu *(Renewable Energies)* kama vile umeme jua, upepo, maporomoko madogo ya maji, jotoardhi na tungamotaka; na kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Nishati, hususan kwenye uzalishaji wa umeme na katika utafiti wa Mafuta na Gesi Asilia.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na maeneo hayo ya Nishati, Wizara pia ilitoa kipaumbele katika Sekta ya Madini hususan

*Chanzo: REA, 2017*

katika: Kuimarisha ukusanyaji wa Mapato ya Serikali yatokanayo na rasilimali za

madini kwa kuziwezesha Ofisi za Madini za Kanda, Ofisi za Afisa Madini Wakazi, Kitengo cha Leseni cha Wizara pamoja na Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA); Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo na wa Kati wa madini; Kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani wa madini; Kuendelea na utafutaji wa *graphite* na madini mengine yanayohitajika kwenye teknolojia ya kisasa *(Rare Earth Elements-REE)*; na Kuimarisha ufuatiliaji na ukaguzi wa afya, usalama, mazingira na uzalishaji wa madini katika migodi midogo, ya kati na mikubwa.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na maeneo hayo ya ki-Sekta, Wizara vilevile iliweka msisitizo katika maeneo mengine yakiwemo: kuwajengea uwezo Watumishi wa Wizara katika fani za Umeme, Mafuta, Gesi Asilia, Jiolojia, Jemolojia, Uhandisi Migodi na Uthaminishaji wa Vito na Almasi; kuelimisha umma na kuboresha mawasiliano kati ya Wizara na wadau mbalimbali kuhusu masuala ya Nishati na Madini; kuboresha mazingira ya Ofisi na vitendea kazi kwa Watumishi; ili kuongeza ufanisi na ubora katika utoaji wa huduma zinazohusu Nishati

na Madini; na kusimamia, kufuatilia na kuboresha Sera, Sheria, Kanuni, Mipango na Miongozo mbalimbali ili kuboresha ufanisi na tija katika Sekta za Nishati na Madini.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara ya Nishati na Madini itaendelea kutekeleza maeneo ya vipaumbele mbalimbali yakiwemo: kuimarisha uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini; kuimarisha ufuatiliaji na ukaguzi wa afya, usalama, mazingira na uzalishaji wa madini katika migodi midogo, ya kati na mikubwa; kuimarisha ukusanyaji wa Mapato ya Serikali yatokanayo na rasilimali za Gesi Asilia na Madini; kusimamia uingizaji, utunzaji na usambazaji wa mafuta nchini; na kuwezesha uwekaji wa mtandao wa usambazaji wa Gesi Asilia viwandani na majumbani pamoja na uendelezaji wa Mradi wa Kusindika Gesi Asilia *(Liquefied Natural Gas - LNG).* Aidha, Wizara pia itatekeleza maeneo mengine mapya ambayo ni pamoja na: kuendelea na utekelezaji wa Mradi Mkubwa wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Kabaale (Uganda) hadi Tanga (Tanzania); Ujenzi wa

*Chanzo: REA, 2017*

Bomba la Mafuta Safi kutoka Dar es Salaam (Tanzania) hadi Ndola (Zambia); Kukamilisha mazungumzo kuhusu ujenzi na upatikanaji wa Gesi Asilia kwenye Viwanda vya Mbolea vinavyotarajiwa kujengwa katika maeneo ya Kilwa Masoko (Lindi) na Mtwara; Kuendelea na ujenzi wa Mradi wa kuzalisha umeme wa Rusumo, **MW 80**; na Kuendelea na utekelezaji wa Agizo la Serikali la kuhamia Dodoma.

***Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali kwa Mwaka 2016/17***

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Nishati na Madini katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 ilipanga kukusanya Jumla ya **Shilingi bilioni 370.68** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 286.66** kwa Mwaka 2015/16. Mapato hayo yanatokana na vyanzo mbalimbali vikiwemo: Ada za kijiolojia; Mrabaha; Ada za Mwaka za Leseni; Mauzo ya Nyaraka za Zabuni; Mauzo ya Gesi Asilia; Tozo ya mauzo ya umeme; na Shughuli za utafiti wa Mafuta na Gesi Asilia. Hadi kufikia mwishoni mwa Mwezi Machi, 2017 Wizara ilikuwa imekusanya Jumla ya **Shilingi bilioni 266.21** sawa na **asilimia 72** ya lengo

*Chanzo: REA, 2017*

lililokusudiwa. Wizara itaendelea na juhudi za kukusanya ili kufikia lengo lililowekwa katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2016/17.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara inatarajia kukusanya Jumla ya **Shilingi bilioni 727.50** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 370.68** kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 kutokana na vyanzo vyake vya mapato, sawa na ongezeko la **asilimia 96.3**. Ongezeko hilo la makisio ya makusanyo limetokana na kuongezeka kwa mchango wa mapato yatokanayo na mauzo ya Gesi Asilia ambayo kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 yalikadiriwa **Shilingi bilioni 115.13** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 477.36** kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18. Kuongezeka kwa mauzo ya Gesi Asilia kutatokana na kuanza kutumika kwa Gesi Asilia katika viwanda vipya vikubwa. Viwanda hivyo ni pamoja na: GOODWILL, Bakhresa Food Products na Lodhia Group vilivyopo Mkuranga - Pwani; Dangote kilichopo Mtwara; pamoja na Coca - Cola na Bidco vilivyopo Kinondoni - Dar es Salaam.

*Chanzo: REA, 2017*

***Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini KwaMwaka 2016/17***

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bajeti iliyopitishwa kwa ajili ya Wizara ya Nishati na Madini pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 ni Jumla ya **Shilingi trilioni 1.122.** Bajeti hiyo inajumuisha Fedha za Miradi ya Maendeleo **Shilingi trilioni 1.056**, sawa na **asilimia 94** ya Bajeti yote ya Wizara. Kati ya fedha hizo za Maendeleo, **Shilingi bilioni 724.84** sawa na **asilimia 68.6** ni fedha za Ndani na **Shilingi bilioni 331.51** sawa na **asilimia 31.4** ni fedha za Nje. Kwa upande wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida, Wizara na Taasisi zake ilitengewa Jumla ya **Shilingi bilioni 66.23**, sawa na **asilimia 6** ya Bajeti yote kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 38.87**, sawa na **asilimia 58.7** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C.) na **Shilingi bilioni 27.36**, sawa na **asilimia 41.3** ni Mishahara kwa ajili ya Idara, Vitengo na Taasisi zilizopo chini ya Wizara.

*Chanzo: REA, 2017*

***Fedha zilizopokelewa hadi Mwezi Mei, 2017***

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 25 Mei, 2017 Wizara ilikuwa imepokea Jumla ya **Shilingi bilioni 591.39**, sawa na **asilimia 52.71** ya Bajeti yote iliyotengwa kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 ambayo ni **Shilingi trilioni 1.122**. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, **Shilingi bilioni 51.64** ni fedha za Matumizi ya Kawaida ambapo Matumizi Mengineyo (O.C.) ni **Shilingi bilioni 28.48** na Mishahara (P.E.) kwa Wizara na Taasisi zake ni **Shilingi bilioni 23.16**. Kiasi kilichopokelewa ni sawa na **asilimia 77.97** ya fedha zote za Matumizi ya Kawaida zilizotengwa ambazo Jumla yake ni **Shilingi bilioni 66.23**.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho Jumla ya **Shilingi bilioni 654.06** ambazo ni fedha za Miradi ya Maendeleo zilipokelewa ambapo fedha za Ndani ni **Shilingi bilioni 522.96** na fedha za Nje ni **Shilingi bilioni 131.1**. Fedha hizo ni sawa na **asilimia 61.93** ya Bajeti yote ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha

*Chanzo: REA, 2017*

wa 2016/17 ambayo ni **Shilingi trilioni 1.056**. Fedha hizo zilizopatikana zilielekezwa katika Miradi ya kupeleka umeme vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA); Mradi wa *Kinyerezi I Extension* (**MW 185**); ulipaji wa deni la Mradi wa Kinyerezi I (**MW 150**); Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme ya Makambako – Songea (kV 220); malipo ya madeni ya TANESCO na Mradi wa Uendelezaji wa Rasilimali za Madini (SMMRP). Aidha, kwa upande wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) hadi kufikia tarehe 25 Mei, 2017 ulikuwa umepokea Jumla ya **Shilingi bilioni 448.87** sawa na **asilimia 76.39** ya Bajeti yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17.

### ***Ufanisi wa Wizara katika Masuala ya Manunuzi***

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia matumizi ya fedha za Umma kwa umakini mkubwa kwa kuhakikisha kuwa masuala ya ununuzi yanafanyika kwa ufanisi mkubwa. Katika

*Chanzo: REA 2017*

ukaguzi wa ununuzi *(Procurement Audit)*

uliofanywa na PPRA katika kipindi cha Mwaka 2015/16, Wizara ya Nishati na Madini imekuwa miongoni mwa Wizara tatu bora kwa kupata **alama ya asilimia 88.85**. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara itaendelea kusimamia manunuzi kwa ufanisi zaidi katika kuhakikisha kuwa fedha za Umma zinatumika ipasavyo kwa maslahi ya maendeleo ya Taifa letu.

## SEKTA YA NISHATI

### SERA, MIPANGO NA SHERIA KATIKA SEKTA YA NISHATI

#### *Mpango Kabambe wa Uendelezaji wa Sekta Ndogo ya Umeme (PSMP) na Matumizi ya Gesi Asilia (NGUMP)*

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2016/17 imekamilisha mapitio ya Mpango Kabambe wa Uendelezaji wa Sekta Ndogo ya Umeme *(Power System Master Plan - PSMP 2016 Update*) ambayo ilikamilika Mwezi Desemba, 2016. Mpango huo umebainisha

*Chanzo: REA, 2017*

utekelezaji wa Miradi ya uzalishaji na usafirishaji wa umeme katika kipindi kifupi (2016 – 2020), kati (2021 - 2025) na kirefu (2026 - 2040). Katika kipindi kifupi, kiasi cha **MW 4,193** zinahitajika, kipindi cha kati **MW 1,280** na kirefu **MW 14,646** zinahitajika kuongezwa ili kuweza kukidhi mahitaji ya umeme nchini.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango huo wa PSMP umezingatia ukuaji wa mahitaji ya umeme nchini, gharama nafuu ya uwekezaji na uchangiaji wa vyanzo mbalimbali vya nishati *(energy mix)* ambapo umeme utazalishwa kutokana na Gesi Asilia, maporomoko ya maji, makaa ya mawe, jua, upepo, jotoardhi na tungamotaka. Mapitio hayo yalifanyika kwa kushirikisha wadau mbalimbali wakiwemo: Wizara na Taasisi za Serikali; Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA); na Sekta Binafsi.

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na mapitio ya PSMP, Wizara pia imeandaa Rasimu ya Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asilia *(Natural Gas Utilization Master Plan – NGUMP)* chini ya ufadhili wa Shirika la

Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA) kwa kushirikisha Taasisi mbalimbali za Serikali, Sekta Binafsi na Wataalam kutoka nchi za Japan pamoja na Trinidad and Tobago. Mpango huu unatoa mwongozo kuhusu matumizi bora ya Gesi Asilia, uboreshaji wa miundombinu ya Gesi Asilia pamoja na kuweka misingi ya kuhakikisha Sekta zote za uchumi zinahusishwa. Mpango huu utatekelezwa kwa kipindi cha Miaka thelathini (30) kuanzia 2017 hadi 2046, ambapo Jumla ya Futi za Ujazo Trilioni 18.7 za Gesi Asilia zimepangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya Soko la Ndani. Aidha, Gesi Asilia kwa ajili ya uzalishaji umeme ndio kipaumbele cha kwanza cha Mpango huu ambapo kiasi cha Gesi Asilia kilichotengwa ni Futi za Ujazo Trilioni 8.3, sawa na **asilimia 44.4** ya Gesi Asilia iliyotengwa kwa ajili ya Soko la Ndani.

*Chanzo: REA, 2017*

***Kanuni za Maboresho na Ushindani katika Sekta Ndogo ya Umeme, Upangaji wa Bei ya Gesi Asilia na Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia***

**23. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekamilisha Kanuni za Maboresho na Ushindani katika Sekta Ndogo ya Umeme za Mwaka 2016 *(The Electricity (Market Re-Organization and Promotion of Competition) Regulations, 2016)* na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali, Na. 229 la tarehe 21 Oktoba, 2016. Kanuni hizo, pamoja na mambo mengine, zinatoa mwongozo wa jinsi ya kuchochea ushindani kwenye shughuli za uzalishaji umeme na kuratibu shughuli hizo kupitia Kamati Maalumu *(Electricity Infrastructure Procurement Coordinator - EIPC).*

**24. *Mheshimiwa Spika,*** Mwezi Oktoba, 2016 Serikali ilikamilisha Kanuni za upangaji wa bei ya Gesi Asilia kwa ajili ya matumizi mbalimbali na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 285. Aidha, kwa kutumia Kanuni hizo ukokotoaji wa

*Chanzo: REA, 2017*

bei za Gesi Asilia kwa ajili ya viwanda vya kimkakati vinavyojumuisha Viwanda vya Mbolea na Saruji ulikamilika Mwezi Januari, 2017. Lengo la upangaji wa bei hizo ni kuhamasisha uwekezaji katika Viwanda vya Mbolea ili kufanikisha upatikanaji wa mbolea ya bei nafuu nchini mwetu.

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia mafanikio yaliyopatikana katika utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia, Serikali imeona upo umuhimu wa kuhakikisha Watanzania wanashiriki katika Tasnia hiyo ipasavyo. Ili kufanikisha azma hiyo, Serikali imeandaa Kanuni Mahsusi zitakazoongoza Kampuni za Mafuta na Gesi Asilia jinsi zitakavyoweza kuwashirikisha Watanzania katika Tasnia ya Mafuta na Gesi Asilia (*Local Content Regulations*). Kanuni husika zimeandaliwa kwa kushirikisha Wadau mbalimbali wakiwemo Taasisi za Umma, Kampuni za Mafuta na Gesi Asilia na Asasi za Kiraia. Kanuni hizo zimekamilika na zimetangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 197 la tarehe 5 Mei, 2017.

*Chanzo: REA, 2017*

**26. *Mheshimiwa Spika*** katika kuhakikisha huduma za udhibiti wa Nishati zinaendelea kufanyika kwa uwazi, ubora na ufanisi kwa lengo la kukuza Uwekezaji na kuboresha Ustawi wa Kijamii na Kiuchumi kwa Jamii ya Watanzania Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) iliandaa Kanuni *(Rules)* mbalimbali. Kanuni hizo ni pamoja na: Kanuni za Uendelezaji na Usimamizi wa Miradi Midogo ya Umeme *(The Electricity (Development of Small Power Projects) Rules, 2016, GN No. 217 of 2016)*; Kanuni za Tozo na Ada za Leseni za Umeme *(The Electricity (Licensing Fees) Rules, 2016, GN No. 287 of 2016)*; Kanuni za Usimamizi wa Mifumo ya Umeme *(The Electricity (System Operation Services) Rules, 2016, GN No. 324 of 2016)*; Kanuni za Usimamizi wa Soko la Biashara ya Umeme *(The Electricity (Market Operation Services) Rules, 2016, GN No. 325 of 2016)*; Kanuni za kusimamia Uuzaji umeme *(The Electricity (Supply Services) Rules, 2017, GN No. 4 of 2017)*; na Usimamizi wa Biashara ya Rejareja ya Petroli Vijijini na kwenye Miji Midogo *(The Petroleum (Retail Operations in Townships and Villages) Rules, 2017, GN No. 14 of 2017)*.

*Chanzo: REA, 2017*

## SEKTA NDOGO YA UMEME

### *Hali ya Upatikanaji wa Umeme Nchini*

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Serikali imeendelea kuboresha Sekta Ndogo ya Umeme kwa kuimarisha hali ya uzalishaji, usafirishaji pamoja na kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme nchini. Umeme uliozalishwa kwa Mwaka 2016 na kuingizwa katika Gridi ya Taifa uliongezeka na kufikia ***GWh* 7,092** ukilinganisha na ***GWh* 6,227** zilizozalishwa Mwaka 2015 sawa na ongezeko la **asilimia 12.20**. Aidha, mahitaji ya juu ya umeme kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 yameongezeka hadi kufikia **MW 1,051.27** iliyofikiwa tarehe 14 Februari, 2017 ukilinganisha na **MW 1,026.02** katika Mwaka 2015/16. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 mitambo yetu ina uwezo wa kuzalisha umeme wa kiasi cha **MW 1,450**.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea na jitihada za makusudi za kuongeza Idadi ya Wananchi wanaopata huduma ya umeme kwa lengo la kushamirisha

*Chanzo: REA 2017*

shughuli za kiuchumi na kijamii. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2017 Idadi ya Wananchi waliofikiwa na huduma ya umeme (*overall electricity access level*) imefikia **asilimia 67.5** kulinganisha na **asilimia 40** iliyokuwa imefikiwa Mwezi Aprili, 2016. Aidha, Idadi ya Wananchi wanaopata huduma ya umeme mijini *(urban electricity access level)* imefikia **asilimia 97.3** ikilinganishwa na **asilimia 63.4** iliyofikiwa Mwaka 2014/15; wakati wanaopata huduma ya umeme vijijini (*rural electricity access level*) imefikia **asilimia 49.5** ikilinganishwa na **asilimia 21** iliyofikiwa Mwaka 2014/15.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na uhakiki ambao ulifanywa na Shirika la Takwimu la Taifa *(National Bureau of Statistics-NBS),* hadi kufikia Mwezi Machi, 2017 imebainika kuwa Idadi ya Wananchi waliounganishiwa umeme (*overall electricity connection level*) imefikia **asilimia 32.8** ikilinganishwa na **asilimia 30** Mwaka 2015/16**.** Aidha, Idadi ya Wananchi waliounganishiwa umeme mijini *(urban electricity connection level)* imefikia **asilimia 65.3** wakati waliounganishiwa umeme vijijini

*Chanzo:: REA, 2017*

(*rural electricity connection level*) imefikia **asilimia 16.9**.

***Kuongeza Uzalishaji wa Umeme***

***Mradi wa Kinyerezi II – MW 240***

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Mradi wa Kinyerezi II unaendelea vizuri. Gharama zote za utekelezaji wa Mradi huu zimeshalipwa. Kazi zifuatazo zimeshafanyika au zinaendelea kufanyika: Mkandarasi SUMITOMO kutoka Japan anaendelea na ujenzi wa miundombinu na misingi *(foundations and concrete beams)* kwa ajili ya kusimika Mitambo sita (6); ujenzi wa Jengo la Ofisi umekamilika na kwa sasa linatumiwa na Wataalam wa SUMITOMO, TOSHIBA na TANESCO; na utengenezaji wa mitambo (*manufacturing*) unaendelea nchini Japan, Korea Kusini na Singapore. Aidha, transfoma nne (4) kati ya nane (8) na Mitambo mitatu (3) kati ya sita (6) iliwasili nchini Mwezi Februari, 2017 ambapo kazi ya kufunga Mitambo imeanza Mwezi Aprili, 2017.

*Chanzo: REA, 2017*

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2017/18 utengenezaji wa Mitambo ya Mradi wa Kinyerezi II viwandani utakamilishwa na kazi ya ufungaji wa Mitambo itaendelea. Aidha, Mtambo wa kwanza wa kuzalisha umeme wa **MW 30** unategemewa kukamilika ifikapo Mwezi Desemba, 2017 na Mradi mzima unatarajiwa kukamilika Mwezi Desemba, 2018.

***Mradi wa Kinyerezi I Extension – MW 185***

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama tunavyofahamu Mradi wa Kinyerezi I **MW 150** ulikamilika na kuanza kuzalisha umeme rasmi Mwezi Machi, 2016. Baada ya Mradi huo kukamilika, Serikali kupitia TANESCO iliingia Makubaliano na Kampuni ya Jacobsen Elektro AS ya Norway ili kupanua Mradi huo kwa kuongeza Mitambo mingine ya **MW 185** (Kinyerezi I *Extension*) na hivyo kufanya uwezo wa Kituo hicho kuwa na Jumla ya **MW 335**. Makubaliano hayo yalitokana na azma ya Serikali ya kuondoa upungufu wa nishati ya umeme kwa kutumia Gesi Asilia inayopatikana nchini mwetu.

**33. *Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizofanyika kwa Mradi wa *Kinyerezi I Extension* ni kukamilisha malipo ya Mkandarasi wa Ufundi, Kampuni ya *Citec* kwa **asilimia 90** na Kampuni ya *General Electric* ya Marekani imekamilisha matengenezo ya Mitambo kwa **asilimia 100** na Mitambo ipo tayari kusafirishwa kuja nchini. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Mkandarasi ataendelea na kazi ya ufungaji wa Mitambo ambapo **Shilingi bilioni 60**, fedha za Ndani zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo. Mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo mwishoni mwa Mwaka 2019.

### *Mradi wa Mto Malagarasi - MW 45*

**34. *Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu unahusisha ujenzi wa Mtambo wa kuzalisha umeme wa **MW 45** kwa kutumia maji ya Mto Malagarasi uliopo Mkoani Kigoma na unatekelezwa na TANESCO. Aidha, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imeonesha nia ya kufadhili Mradi huu. Taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi wa Mradi zinaendelea

*Chanzo: REA, 2017*

ambapo kwa sasa uchambuzi wa zabuni unafanyika na unatarajiwa kukamilika Mwezi

Mei, 2017. Gharama za utekelezaji wa Mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 149.5**, sawa na takriban **Shilingi bilioni 345.49** na unatarajiwa kukamilika Mwaka 2020. Katika Mwaka wa Fedha 2017/18, Serikali imetenga kiasi cha **Shilingi bilioni 2.8** kwa ajili ya kuanza kugharamia utekelezaji wa Mradi huu.

***Mradi wa Kakono - MW 87***

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu unahusu ujenzi wa Mtambo wa kuzalisha umeme wa **MW 87** kwa kutumia maji ya Mto Kagera uliopo Mkoani Kagera na unatekelezwa na TANESCO. Serikali imewasilisha maombi ya Mkopo kwa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) Mwezi Julai, 2016 kwa ajili ya kutekeleza Mradi huu ambapo AfDB wameonesha nia ya kuufadhili. Mshauri Mwelekezi Kampuni ya *SP Studio Pietrangeli* ya Italia amepatikana kwa ajili ya usimamizi wa Mradi.

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inakamilisha taratibu za kubadilisha umiliki

*Chanzo: REA, 2017*

wa eneo la Mradi wa Kakono lenye ukubwa wa Hekta 1,100 kutoka kwa Wamiliki wa sasa (NARCO na Kagera Sugar) kwenda TANESCO. Maombi yamewasilishwa kwa Mamlaka husika za Wilaya za Misenyi na Karagwe ili kupima na kutambua mipaka ya eneo la Mradi. Gharama za ujenzi wa Mtambo na njia ya usafirishaji umeme ni **Dola za Marekani milioni 379.4,** sawa na takriban **Shilingi bilioni 876.79** na Mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo Mwaka 2021. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza Mradi huo kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 ni **Shilingi bilioni 2.05** ambazo ni fedha za Nje.

***Mradi wa Rusumo - MW 80***

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu wa Rusumo wa **MW 80,** Tanzania itapata **MW 26.6**. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Wakandarasi wa kujenga Kituo cha kufua umeme, *COCO Group Jingal Water* (China) *and Hydropower Construction Company* (Canada), walisaini Mkataba tarehe 9 Novemba, 2016. Wakandarasi hao watahusika na kazi za "C*ivil and Hydro-mechanical*". Pamoja nao watakuwepo

*Chanzo: REA 2017*

*Andritz Hydro GmbH and Andritz Hydro PVT Ltd* kutoka nchi ya Austria watakaohusika na kazi za *Electro-mechanical*. Aidha, malipo ya awali kwa Wakandarasi kiasi cha **Dola za Marekani milioni 16.3** sawa na takriban **Shilingi bilioni 37.67** yamefanyika na utekelezaji wa Mradi unaendelea.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** uzinduzi rasmi wa kuanza ujenzi *(Ground breaking ceremony)* wa Kituo cha kufua umeme cha Rusumo ulifanywa na Mawaziri wanaosimamia masuala ya Nishati wa nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi, pamoja na Benki ya Dunia (WB) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) tarehe 30 Machi, 2017. Gharama za ujenzi wa Mtambo wa kufua umeme ni **Dola za Marekani milioni 340** sawa na takriban **Shilingi bilioni 785.74**. Mchango wa Serikali ni **Dola za Marekani milioni 113** ambao ni Mkopo kutoka Benki ya Dunia (WB). Kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, kiasi cha **Shilingi bilioni 2.8** kimetengwa kugharamia shughuli za ujenzi wa Kituo hicho na Mradi unatarajiwa kukamilika Mwaka 2020.

*Chanzo: REA, 2017*

***Mradi wa Somanga Fungu (Lindi) - MW 300***

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza kiwango cha uzalishaji wa umeme nchini, Serikali imepanga kuongeza Mitambo ya kuzalisha umeme ya **MW 300** kwa kutumia Gesi Asilia katika eneo la Somanga Fungu Wilaya ya Kilwa, Mkoani Lindi. Upembuzi Yakinifu wa Mradi ulikamilika Mwezi Oktoba, 2016 kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia. Hatua inayofuata ni kutangazwa kwa Mradi ili kupata Mtekelezaji *(EPC & Financing)* atakayeshirikiana na Serikali kutekeleza Mradi unaokadiriwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 423,** sawa na takriban **Shilingi bilioni 977.55** na unatarajiwa kukamilika Mwaka 2020.

***Mradi wa Somanga Fungu - MW 240.***

***40.*** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kuongeza kiwango cha uzalishaji wa umeme nchini, Serikali kupitia TANESCO imepanga kutekeleza mradi wa **MW 240** kwa kutumia

*Chanzo: REA, 2017*

gesi asilia. Mradi huu utatekelezwa katika eneo la Somanga Fungu, Kilwa kwa utaratibu

wa *EPC with financing* kupitia Kampuni ya Sumitomo ya Japan. Gharama za kutekeleza mradi huu zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani Milioni 300** ambapo asilimia 85 itatolewa na Benki ya Japan *(Japan Bank for International Cooporation - JBIC)* na asilimia 15 ya fedha hizo itatolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

***41. Mheshimiwa Spika,*** kazi ya upembuzi yakinifu wa mradi huu inaendelea na inatarajiwa kukamilika baada ya miezi mitatu (3). Kazi yote ya ujenzi inatarajiwa kufanyika ndani ya miaka miwili (2) na mradi unatarajiwa kukamilika Mwaka 2020. Mradi huu utamilikiwa na Serikali.

***Mradi wa Kufua Umeme Mtwara - MW 300***

***42. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TANESCO ilianza majadiliano na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Ushirikiano wa Kimataifa (JICA) kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa kutumia Gesi Asilia wa **MW 300**. Mradi huu utahusisha ujenzi wa Mitambo ya kufua umeme na njia ya kusafirisha umeme

*Chanzo: REA, 2017*

ya msongo wa **kV 400** kutoka Mtwara hadi Somanga Fungu.

***43. Mheshimiwa Spika,*** Kazi zinazoendelea kwa sasa ni upembuzi yakinifu na baada ya hapo TANESCO itafanya majadiliano ya kiufundi na kifedha. Utekelezaji wa mradi huo utaimarisha upatikanaji wa umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara pamoja na kuingiza Mikoa hiyo katika Gridi ya Taifa. Aidha, ujenzi huo utawezesha kuuza umeme wa ziada nchi za jirani ikiwemo Msumbiji. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Mwaka 2020 na utamilikiwa na Serikali.

***Mradi wa Umeme wa Makaa ya Mawe Kiwira - MW 200***

***44. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia STAMICO imeanza majadiliano na Serikali ya Urusi ambayo imeonesha nia ya kufadhili utekelezaji wa Mradi wa Kiwira kwa ajili ya kuzalisha umeme wa **MW 200** kwa kutumia Makaa ya Mawe pamoja na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **kV 400** kutoka Kiwira hadi Kituo cha Mwakibete

*Chanzo: REA 2017*

(Mbeya) na kuingizwa katika Gridi ya Taifa. Kazi zitakazofanyika Mwaka 2017/18 ni pamoja na kukamilisha majadiliano na Mwekezaji na kuendelea kuchimba makaa ya mawe. Gharama ya Mradi wote inakaridiwa kuwa **Dola za Marekani milioni 440**.

***Miradi ya Kinyerezi III - MW 600 na Kinyerezi IV - MW 330***

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** Miradi hii imepangwa kutekelezwa chini ya Mpango wa ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi (PPP). Aidha, Majadiliano ya utekelezaji wa Miradi yamechukua muda mrefu kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo Wabia kuhitaji dhamana ya Serikali *(Goverment Guarantee)*; Mwekezaji kutaka Serikali iingie Makubaliano ya moja kwa moja na Wakopeshaji *(Direct Agreement with Lenders);* Mfumo wa utekelezaji miradi kati ya *Build Own and Operate (BOO)* na *Build Own Operate and Transfer (BOOT)* kwa miradi ya IPP, na Bei ya umeme *(tariff)* zinazopendekezwa na Wawekezaji kuwa za juu kuliko bei elekezi zinazotolewa na EWURA.

*Chanzo: REA 2017*

**46. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kusisitiza kuwa Mfumo wa utekelezaji miradi utumike wa *Build Own and Operate (BOO)* au *EPC & Financing* ambapo hakutakuwa na *Government Guarantee*, *Capacity Charge* wala *Minimum Off - Take.* Aidha, *CAPEX (Investment cost*) isiwe sehemu ya formula itakayotumika kupata bei ya umeme (*tariff)* na TANESCO italipia gharama za *energy component (variable Operation and Maintenance cost - O&M)*.

***Miradi ya Uzalishaji Umeme ya Sekta Binafsi***

**47. *Mheshimiwa Spika,*** upande wa Miradi ya Uzalishaji Umeme inayotekelezwa na Sekta Binafsi (IPP) ikiwemo Mradi wa Somanga Fungu **MW 320** wa Kilwa *Energy;* Mradi wa Mchuchuma **MW 600;** na Ngaka **MW 400** chini ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) bado ipo katika hatua mbalimbali za majadiliano.

*Chanzo: REA, 2017*

***Upanuzi na Uboreshaji wa Njia za Usafirishaji wa Umeme***

***Mradi wa Msongo wa kilovolti 400 kutoka Iringa hadi Shinyanga (Backbone Transmission Investment Project - BTIP)***

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa njia ya umeme wa Msongo wa kilovolti 400 na upanuzi wa Vituo vya kupozea umeme kutoka Iringa – Dodoma – Singida – Tabora - Shinyanga ulikamilika Mwezi Desemba, 2016 kwa **asilimia 100**. Kwa sasa umeme unasafirishwa kwa kutumia njia hiyo na kupelekea kuboresha upatikanaji wa umeme katika maeneo ya Mikoa hiyo na kwenye Gridi ya Taifa kwa ujumla. Uzinduzi rasmi wa Mradi huu utafanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***Mradi wa Msongo wa kilovolti 220 kutoka Makambako hadi Songea na Usambazaji wa Umeme Vijijini kwa Mikoa ya Njombe na Ruvuma***

*Chanzo: REA 2017*

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme

wa Msongo wa kV 220 kutoka Makambako hadi Songea yenye urefu wa kilomita 250, ujenzi wa Vituo Vipya vya kupozea umeme eneo la Madaba na Songea, umeme wa Msongo wa kV 220/33 na upanuzi wa Kituo cha kupozea umeme cha Makambako. Kwa upande wa njia ya kusafirisha umeme kV 220 Makambako – Songea, Mkandarasi amekamilisha manunuzi ya vifaa vya Mradi na usimikaji wa nguzo umeanza Mwezi Machi, 2017.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa ujenzi wa Vituo vitatu (3) vya kupoza umeme vyenye uwezo wa kV 220/33 katika maeneo ya Makambako, Madaba na Songea, Wakandarasi Kampuni za Shandong Taikai na Norino International za China zinaendelea kupima sampuli za udongo na kusawazisha maeneo ya kujenga Vituo hivyo na ujenzi utaanza Mwezi Mei, 2017. Aidha, kwa upande wa kazi ya usambazaji umeme, Mkandarasi Kampuni ya Isolux Ingenieria S.A ya Hispania inaendelea na kazi ya kusimika nguzo na kuvuta nyaya ambapo hadi kufikia Mwezi Aprili, 2017 amekamilisha umbali wa kilomita 365 kati ya 580, sawa na **asilimia**

*Chanzo: REA, 2017*

**62.9** katika maeneo ya Mkoa wa Ruvuma. Kwa upande wa Makambako hadi Njombe usimikaji wa nguzo na kuvuta nyaya umefikia kilomita 118 kati ya kilomita 393, sawa na **asilimia 30**. Aidha, Kituo kidogo cha kupozea umeme cha Songea kV 33/11 kimekamilika kwa **asilimia 52**.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Wakandarasi Shandong Taikai na Norino International za China wataendelea na kazi za kukamilisha ujenzi wa Vituo vya kupoza umeme na Kampuni ya Kalpataru *Power Transmission* Ltd ya India itaendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Makambako hadi Songea. Aidha, Kampuni ya Isolux ya Hispania itaendelea na ujenzi wa njia ya usambazaji umeme na kuunganisha vijiji vilivyopo kati ya Makambako hadi Songea kwenye Mkuza wa njia ya usafirishaji umeme. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Mradi umetengewa **Shilingi bilioni 3** fedha za Ndani ikiwa ni mchango wa Serikali na **Shilingi bilioni 8** ikiwa ni fedha za Nje kutoka Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la Maendeleo la Kimataifa (Sida). Utekelezaji wa

*Chanzo: REA, 2017*

Mradi huu unatarajiwa kukamilika Mwezi Agosti, 2018.

***Mradi wa Njia ya Umeme ya Msongo wa kilovolti 400 wa Singida – Arusha – Namanga***

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatekeleza Miradi ya ushirikiano wa ki-Kanda ikiwemo Mradi wa njia ya kusafirisha umeme Singida – Arusha – Namanga kV 400. Kazi zilizofanyika katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 ni pamoja na: TANESCO kusaini Mkataba na Kampuni ya Kalpataru Power Transmission Ltd kutoka nchini India kwa ajili ya ujenzi wa njia ya umeme kutoka Singida hadi Babati (km 150), Kampuni ya Bouygues Energy & Services ya Ufaransa kwa ajili ya ujenzi wa njia ya umeme kutoka Babati hadi Arusha (km 150) na Kampuni ya Ubia kati ya Energoinvest ya Yugoslavia na EMC ya India kwa ajili ya ujenzi wa njia ya umeme kutoka Arusha hadi Namanga (km 114); na kukamilika kwa tathmini ya athari za mazingira na mali za Wananchi watakaopisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme.

*Chanzo: REA, 2017*

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** taratibu za kupata Mkandarasi wa ujenzi wa Kituo kipya cha Arusha cha Msongo wa kV 400/220 na upanuzi wa Kituo cha Singida zimekamilika. TANESCO inatarajia kusaini Mkataba na Kampuni ya Ubia kati ya Energoinvest ya Yugoslavia na EMC ya India ambayo imeshinda zabuni Mwezi Aprili, 2017. Aidha uchambuzi wa zabuni za Wakandarasi wa usambazaji umeme vijijini umeanza. Gharama za Mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 258.82**, sawa na takriban **Shilingi bilioni 598.13**. Fedha hizi zinatolewa na AfDB, JICA na Serikali ya Tanzania ambayo itachangia **Dola za Marekani milioni 43.89**, sawa na takriban **Shilingi bilioni 101.43**.

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizofanyika katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 ni pamoja na kukamilisha taratibu za malipo ya fidia na kuanza kutekeleza Mradi kwa awamu. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Serikali imetenga fedha za Ndani **Shilingi bilioni 48** kwa ajili ya ulipaji wa fidia. Aidha, utekelezaji wa Mradi utaanza baada ya ulipaji wa fidia kukamilika na Wakandarasi kulipwa malipo ya awali.

*Chanzo: REA, 2017*

Mradi huu unatarajiwa kukamilika Mwezi Desemba, 2019.

***Mradi wa North - West wa kilovolti 400 kutoka Mbeya – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma – Nyakanazi***

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 kazi ambazo zimefanyika ni pamoja na: kudurusu Upembuzi Yakinifu wa Mradi kutoka Msongo wa kV 220 na kuwa kV 400 kwa eneo la Mbeya hadi Nyakanazi lenye urefu wa kilomita 1,080; utafiti wa athari za mazingira kwa Awamu ya Pili kutoka Nyakanazi – Kigoma - Mpanda, kilomita 568 ambao umekamilika Mwezi Februari, 2017; na kuanza Majadiliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Korea ya Kusini kupitia Shirika lake la Maendeleo *(EDCF)* na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ajili ya kupata fedha za utekelezaji wa Mradi. Hatua iliyofikiwa ni kwamba tayari Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango imewasilisha maombi rasmi kwa Taasisi hizo ya **Dola za Marekani milioni 428** sawa na takriban **Shilingi bilioni 989.11**.

*Chanzo: REA, 2017*

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kukamilisha taratibu za upatikanaji wa fedha za kutekeleza sehemu ya Mradi huo kutoka Nyakanazi hadi Kigoma kwa ufadhili wa EDCF ya Korea Kusini ambayo imeonesha nia ya kutoa Mkopo wa masharti nafuu wa **Dola za Marekani milioni 50**, sawa na takriban **Shilingi bilioni 115.55**; kukamilisha utafiti wa athari za mazingira kutoka Mpanda hadi Sumbawanga; na kulipa fidia Wananchi kutoka Nyakanazi hadi Kigoma ambapo **Shilingi bilioni 12.3** zimetengwa katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18.

***Mradi wa North - East wa kilovolti 400 kutoka Kinyerezi hadi Arusha kupitia Chalinze na Segera***

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu una lengo la kusafirisha umeme kutoka Kituo cha Kinyerezi, Dar es Salaam hadi Arusha kwa lengo la kukidhi mahitaji ya umeme kwenye Gridi ya Taifa hususan katika Mikoa ya Pwani, Tanga, Kilimanjaro na Arusha. Gharama ya Mradi huu ni takriban **Dola za**

*Chanzo: REA, 2017*

**Marekani milioni 692.7**, sawa na takriban **Shilingi trilioni 1.6** ambapo Benki ya Exim ya China itatoa Mkopo wa **asilimia 85** na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itatoa **asilimia 15** ya gharama za Mradi.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 kazi zilizofanyika kwenye Mradi huu ni pamoja na: kusainiwa kwa Mkataba wa Mkopo na pande husika Mwezi Agosti, 2016; kusainiwa kwa Mkataba kati ya TANESCO na Mtaalamu Mshauri Kampuni ya TBEA kutoka China kwa ajili ya usimamizi wa Mradi Mwezi Januari, 2017; na kukamilika kwa tathmini ya mali kwa maeneo ya kujenga Vituo vya kupoza umeme vya Segera na Tanga pamoja na eneo la njia ya umeme kutoka Kinyerezi hadi Kiluvya, Dar es Salaam.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 kazi zilizopangwa kufanyika kwenye Mradi huu ni kukamilisha tathmini ya mali za Wananchi watakaopisha sehemu ya Mradi, pamoja na kulipa fidia kwa Awamu ya Kwanza kutoka

*Chanzo: REA, 2017*

Kinyerezi hadi Chalinze. Serikali imetenga fedha za Ndani kiasi cha **Shilingi bilioni 19.80** kwa ajili ya kulipa fidia kwa Waathirika pamoja na mchango wa sehemu ya **asilimia 15** ya gharama ya Mradi.

***Mradi wa njia ya umeme ya Msongo wa kilovolti 400 kutoka Somanga Fungu hadi Kinyerezi***

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka eneo la Somanga Fungu Mkoani Lindi hadi Kinyerezi Mkoani Dar es Salaaam pamoja na ujenzi wa Kituo cha kupoza umeme eneo la Somanga Fungu. Njia hii itatumika kusafirisha umeme utakaozalishwa na Mitambo yenye uwezo wa kufua takriban **MW 620** inayotarajiwa kujengwa eneo la Somanga Fungu Kilwa Mkoani Lindi. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 TANESCO imesaini Mkataba na Mtaalam Mshauri Kampuni ya Byucksan Power Ltd ya Korea Kusini ili kudurusu Upembuzi Yakinifu na kusimamia ujenzi wa njia ya kusafirishia umeme; na kulipa fidia

*Chanzo: REA, 2017*

kwa Wananchi wanaopisha ujenzi wa njia hiyo. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2017 ulipaji wa fidia kwa mali za Waathirika wa Mradi ulikuwa umefanyika kwa Waathirika 2,305 kati ya 3,901 (sawa na **asilimia 59.1**) kwa kiasi cha **Shilingi bilioni 46.29.**

***Mradi wa njia ya Umeme wa Msongo wa kilovolti 220 kutoka Kituo cha Kufua Umeme* wa *Maji cha Rusumo hadi Nyakanazi***

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Rusumo wa **MW 80** unahusisha ujenzi wa njia za kusafirisha umeme kutoka Rusumo, Mto Kagera hadi kwenye Gridi ya nchi za Burundi, Rwanda na Tanzania. Kwa upande wa Tanzania, Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Kituo cha kuzalisha umeme cha Rusumo hadi Nyakanazi yenye urefu wa kilomita 98 kwenye Msongo wa kV 220. Mradi huu utasaidia kuunganisha Mikoa ya Kagera, Kigoma, Rukwa na Katavi kwenye Mfumo wa Gridi ya Taifa na kuipatia umeme mwingi zaidi na wa uhakika.

*Chanzo: REA, 2017*

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2016/17 kazi zilizofanyika kwenye Mradi huu ni pamoja na: kusainiwa kwa Mkataba Mwezi Desemba, 2016 kati ya TANESCO na Mtaalam Mshauri, Kampuni za WSP Canada Inc. na GOPA *International Energy Consultant GmbH* ya Ujerumani kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Mradi; upimaji wa njia na kufanya tathmini ya fidia ya mali za Wananchi watakaopisha eneo la Mradi. Aidha, Serikali imewasilisha taarifa ya Upembuzi Yakinifu Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) Mwezi Februari, 2017 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha kupoza umeme eneo la Benaco lililopo Wilayani Ngara, Mkoani Kagera.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 kazi zitakazofanyika kwenye Mradi huu ni: kukamilisha ulipaji wa fidia kwa Waathirika wa Mradi na kuwapata Wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme pamoja na Kituo cha kupoza umeme cha Benaco Wilayani Ngara, Mkoani Kagera. Serikali imetenga kiasi cha **Shilingi bilioni 5.2** fedha za Ndani kwa ajili ya kulipa fidia.

*Chanzo: REA, 2017*

***Mradi wa Njia ya umeme ya Msongo wa kilovolti 220 kutoka Bulyanhulu hadi Geita***

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi utahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa Msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita 55 pamoja na usambazaji umeme katika vijiji vinavyopitiwa na Mradi Wilayani Geita. Mradi huu unatekelezwa kwa Mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Kiarabu *(Arab Bank for Economic Development in Africa - BADEA), OPEC Fund for International Development* (OFID) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kazi zilizofanyika kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 ni kukamilisha uchambuzi wa zabuni za kuwapata Wakandarasi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme Mwezi Februari, 2017 na tathmini ya mali za Wananchi watakaopisha eneo la Mradi.

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 kazi zitakazofanyika kwenye Mradi huu ni kulipa fidia kwa Wananchi watakaopisha eneo la Mradi na pia kuanza ujenzi. Fedha za Nje zilizotengwa

*Chanzo: REA 2017*

kwa ajili ya kutekeleza Mradi huu ni **Shilingi bilioni 7** na fedha za Ndani ni **Shilingi bilioni 1** kwa ajili ya kulipa fidia.

***Mradi wa Njia ya umeme ya Msongo wa kilovolti 220 kutoka Geita hadi Nyakanazi***

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa Msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita 133, Kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi na kusambaza umeme kwenye vijiji vinavyopitiwa na Mradi. Aidha, Mradi huu utagharimu takriban **Euro milioni 45** sawa na **Shilingi bilioni 95.67** kwa ufadhili wa KfW ya Ujerumani, AFD ya Ufaransa, Jumuiya ya Ulaya (EU) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizofanyika kwenye Mradi huu kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 ni pamoja na: upimaji wa njia kuu ya usafirishaji umeme kutoka Geita hadi Nyakanazi; tathmini ya gharama ya fidia kwa mali za Wananchi watakaoathirika;

*Chanzo: REA, 2017*

tathmini ya athari ya kijamii na mazingira; pamoja na usanifu wa Mradi.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 kazi zitakazofanyika kwenye Mradi huu ni pamoja na kukamilisha ulipaji wa fidia kwa Wananchi watakao-athirika pamoja na kuanza utekelezaji wa Mradi. Fedha za Nje zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza Mradi huu ni Jumla ya **Shilingi bilioni 9.1** ambapo **Shilingi bilioni 1.6** ni fedha za Nje na fedha za Ndani ni **Shilingi bilioni 7.5** kwa ajili ya kulipa fidia.

***Miradi ya Usambazaji wa Umeme***

***Mradi wa kuboresha Mfumo wa usambazaji umeme katika Jiji la Dar es Salaam chini ya Ufadhili wa JICA***

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu ulihusisha kazi zifuatazo: ukarabati wa Kituo cha Ilala kV 132/33/11; ujenzi wa Jengo Jipya la "*Control Center*" la Ilala; ufungaji wa njia ya pili ya usafirishaji umeme wa Msongo wa kV 132 kutoka Ubungo hadi Ilala; kupanua Kituo cha kupoza umeme cha

*Chanzo: REA 2017*

Msasani kV 33/11; ujenzi wa Vituo Vipya vinne (4) vya kupoza umeme wa kV 33/11 vya Jangwani *Beach,* Mwananyamala, Msasani na Muhimbili; ujenzi wa njia mpya za Msongo wa kV 33 kutoka Vituo vya kupoza umeme vya Makumbusho, *City Centre* na Tegeta kwenda Vituo Vipya vya Mwananyamala, Muhimbili, Jangwani na Msasani.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Mradi huu ulifadhiliwa na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo la JICA kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 38**, sawa na takriban **Shilingi bilioni 87.82** na utekelezaji wake umekamilika kwa **asilimia 100** Mwezi Machi, 2017. Mradi huu unasubiri kuzinduliwa rasmi na Viongozi wa Kitaifa.

***Mradi wa Kuboresha Mfumo wa Usambazaji Umeme katika Manispaa ya Dodoma chini ya Ufadhili wa JICA***

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TANESCO ipo katika majadiliano na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake

*Chanzo: REA, 2017*

la Ushirikiano la Kimataifa (JICA) katika utekelezaji wa Mradi wa kuboresha mfumo wa Usambazaji Umeme katika Manispaa ya Dodoma. Mradi huu utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV 132 yenye urefu wa kilometa 135 kutoka Zuzu kwenda Msalato na Kikombo na ujenzi wa Vituo viwili (2) vya kupoza umeme vyenye uwezo wa MVA 90 kila kimoja katika maeneo ya Msalato na Kikombo. Kazi nyingine itakuwa ni ujenzi wa njia za kusambaza umeme za msongo wa kV 33 zenye urefu wa kilometa 71 katika Manispaa ya Dodoma.

**72.** ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa Mradi huu utaimarisha upatikanaji wa umeme katika Manispaa ya Dodoma na vitongoji vyake na pia kukidhi mahitaji ya umeme yatakayoongezeka kutokanaa na Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi. Aidha, Mradi huu unatarajiwa kuanza Mwaka wa fedha 2018/19 na utagharimu **Dola za Marekani milioni 38** sawa na takriban **Shilingi bilioni 76**.

*Chanzo: REA, 2017*

***Mradi wa TEDAP wa Kuboresha Njia za Usambazaji Umeme (Distribution) Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Kilimanjaro chini ya Ufadhili wa Benki ya Dunia***

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu unahusisha upanuzi na ujenzi wa Vituo Vipya 19 vya kupoza umeme wa Msongo wa kV 33/11 pamoja na ujenzi wa njia za usambazaji umeme kwa Msongo wa kV 33 na kV 11 zenye urefu wa kilomita 107 na kilomita 34.01 sawia katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Kilimanjaro kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 43**, sawa na takriban **Shilingi bilioni 99.37**. Fedha hizi zimetolewa na Benki ya Dunia kupitia Mradi wake wa TEDAP.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa Mradi huu upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo hadi kufikia Mwezi Aprili, 2017 **asilimia 85** ya kazi zote zilizopangwa zilikamilika na matarajio ni kukamilisha Mradi huo ifikapo Mwezi Juni, 2017.

*Chanzo: REA, 2017*

***Mradi wa uboreshaji wa huduma za umeme Jijini Dar es Salaam chini ya Ufadhili wa Finland***

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu ulihusisha uboreshaji wa miundombinu ya umeme katika Jiji la Dar es Salaam kwa kufanya yafuatayo: kujenga Kituo kipya cha kupoza umeme cha Msongo wa kV 132/33; kufunga Kangavuke mbili (2) zenye uwezo wa MVA 50 kila moja kwenye Kituo cha *City Centre*; kujenga njia ya umeme wa Msongo wa kV 132 chini ya ardhi kutoka Kituo cha Ilala hadi Kituo kipya cha *City Centre*; kujenga njia ya mzunguko wa umeme *(ring circuit)* chini ya ardhi wa Msongo wa kV 33 kutoka Kituo cha kupoza umeme cha *City Centre* kwenda Sokoine – *Railway* – Kariakoo na kurudi tena *City Centre*; pamoja na kuanzisha Kituo cha kuongozea Mifumo ya Usambazaji umeme katika Msongo wa kV 33 na kV 11 *(Distribution SCADA)* katika eneo la Mikocheni.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu ulifadhiliwa na Serikali ya Finland kwa gharama ya **Euro milioni 21.8** na **Dola za**

*Chanzo: REA, 2017*

**Marekani milioni 1.5** sawa na takriban **Shilingi bilioni 3.47**. Kituo cha kuongozea Mifumo ya Usambazaji umeme katika Msongo wa kV 33 na kV 11 *(Distribution SCADA)* kilichopo Mikocheni **kilizinduliwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)** tarehe 16 Novemba, 2016. Mradi huo ulikamilika Mwezi Februari, 2017.

***Mradi wa ORIO kwa Miji ya Ngara, Biharamulo na Mpanda***

**77. *Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu unahusisha ufungaji wa Mitambo ya kufua umeme yenye uwezo **MW 2.5** kwa kila Wilaya za Biharamulo, Mpanda na Ngara na kupanua njia za usambazaji umeme kwa lengo la kuyapatia maeneo husika umeme wa uhakika. Gharama ya Mradi ni **Euro milioni 33.5** sawa na **Shilingi bilioni 71.22** kupitia ufadhili wa Serikali ya Uholanzi iliyotoa **asilimia 50** na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyotoa **asilimia 50**.

*Chanzo: REA, 2017*

**78. *Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu umekamilika kwa Wilaya ya Biharamulo Mwezi Septemba, 2016 na Wilaya ya Ngara Mwezi Desemba, 2016. Mafunzo ya Wajasiriamali katika maeneo ya Mradi na mafunzo ya afya na usalama kazini kwa Wafanyakazi wa TANESCO katika Vituo hivi vya umeme vya Biharamulo, Mpanda na Ngara yamefanyika Mwezi Machi, 2017. Kazi inayoendelea kwa sasa ni ufungaji wa Mitambo ya kufua umeme na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme katika Wilaya ya Mpanda ambapo unatarajia kukamilika Mwezi Juni, 2017.

***Mradi wa TANESCO wa Urban Electrification***

**79. *Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu unahusu usambazaji umeme kwa Wateja ambao hawajaunganishwa na umeme maeneo ya mijini *(urban electrification programme)*. Aidha, Mradi wa njia ya kusafirisha umeme ya Msongo wa kilovolti 132 kutoka Morogoro hadi Mtibwa umeingizwa kama sehemu ya utekelezaji wa Mradi huu. Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imeonesha nia ya

*Chanzo: REA, 2017*

kufadhili Mradi huu kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 222.62** sawa na takriban **Shilingi bilioni 514.47**.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazofanyika kwenye Mradi huu kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 ni pamoja na: TANESCO kuboresha Upembuzi Yakinifu *(feasibility study)* ikihusisha Mradi wa Morogoro – Mtibwa wa kV 132; Serikali kusaini Mkataba wa Ufadhili na AfDB; na baadae kuanza utekelezaji wa Mradi.

**Miradi ya Kusambaza Umeme Vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA)**

**(i)** ***Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Pili (REA Turnkey Phase II)***

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kufanikisha azma ya Serikali ya kuhakikisha kuwa Wananchi wengi zaidi wanapata huduma za umeme, Serikali ilitekeleza Mradi Kabambe wa Awamu ya Pili ***(REA Turnkey Phase II)*** wa Kusambaza Umeme Vijijini katika Mikoa yote ya Tanzania Bara. Katika

*Chanzo: REA, 2017*

kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Wakala ulikamilisha kazi zifuatazo: ujenzi wa Vituo sita (6) vya kuongeza nguvu ya umeme kutoka Msongo wa kV 11 hadi 33 katika Miji ya Kasulu, Kibondo, Kigoma, Mbinga, Ngara na Tunduru; ujenzi wa njia za kusambaza umeme za Msongo wa kV 33 zenye urefu wa kilomita 17,740; ujenzi wa Vituo Vidogo vya kupoza na kusambaza umeme 4,100; na ujenzi wa njia ndogo ya usambazaji umeme zenye urefu wa kilomita 10,970. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2017, Wateja wa awali 153,821 sawa na **asilimia 62** walikuwa wameunganishiwa umeme kati ya Wateja 250,000 waliopangwa kuunganishwa. Aidha, kazi za kuunganisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya 13 za Busega, Buhigwe, Chemba, Itilima, Kakonko, Kalambo, Kyerwa, Mkalama, Mlele, Momba, Nanyumbu, Nyasa, na Uvinza zimekamilika na kufanya Jumla ya Makao Makuu ya Wilaya zilizopelekewa umeme kupitia Miradi ya REA kufikia 25. Gharama za Mradi wa huu ni **Shilingi bilioni 900.15** zote zikiwa ni fedha za Ndani.

*Chanzo: REA, 2017*

### (ii) *Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu (REA Turnkey Phase III)*

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Mwezi Agosti, 2016 Vijiji 4,395 vilikuwa vimefikiwa na umeme sawa na **asilimia 36** ya vijiji 12,268 vilivyopo Tanzania Bara. Lengo la Serikali ni kufikia Vijiji 7,873 vilivyosalia ifikapo Mwaka 2020/21. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 maandalizi ya Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu yamekamilika na utekelezaji umeanza. Mradi huu ni wa miaka mitano (5) kuanzia 2016/17 hadi 2020/21 na unalenga kufikisha huduma ya umeme kwenye vijiji vyote nchini ambavyo bado havijafikiwa na umeme. Mradi unahusisha: kuongeza wigo wa usambazaji umeme kwenye maeneo yaliyofikiwa na miundombinu ya umeme *(Densification)*; kufikisha umeme wa Gridi kwenye vijiji ambavyo havijafikiwa na umeme *(Grid extension);* na Miradi ya umeme ya nje ya Gridi *(off-grid)* utokanao na Nishati Jadidifu, hasa Umeme Jua *(Solar power).*

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua zilizofikiwa katika maandalizi na utekelezaji ni pamoja na kukamilika kwa uandaaji

*Chanzo: REA 2017*

wa orodha ya vijiji ambavyo havijapatiwa umeme; kusainiwa Mikataba na kuanza utekekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya Mradi wa *Densification* Mwezi Desemba, 2016 unaohusisha Mikoa ya Arusha, Iringa, Mara, Mbeya, Pwani na Tanga kwa ufadhili wa Serikali ya Norway kwa kiasi cha **Shilingi bilioni 28.62**. Aidha, taratibu za upatikanaji wa Wakandarasi wa kusambaza umeme kwenye vijiji vilivyo kwenye Mkuza wa njia ya kusafirisha umeme wa *Backborne Transmission Investment Project (BTIP)* kutoka Iringa hadi Shinyanga umekamilika na Mradi umeanza kutekelezwa Mwezi Januari, 2017. Vilevile, uchambuzi wa maombi 300 ya kusambaza umeme wa Nishati Jadidifu kwa vijiji vilivyo nje ya Gridi ya Taifa umekamilika na utekelezaji wake utaanza Mwezi Julai, 2017.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali itaendelea na utekelezaji kwa kufikisha umeme katika vijiji 3,559 ambavyo tayari Wakandarasi walishaanza kazi. Aidha, Serikali kupitia REA itakamilisha taratibu za ununuzi wa Wakandarasi kwa ajili ya kufikisha umeme kwenye vijiji 4,314 vilivyosalia ambavyo

*Chanzo: REA, 2017*

vinajumuisha vijiji ambavyo vitapatiwa umeme wa nje ya Gridi *(off-grid).* Aidha, Serikali itaendelea na kusambaza umeme kwenye vijiji vilivyo pembezoni mwa Mkuza wa njia ya kusafirisha umeme wa *Backborne Transmission Investment Project (BTIP)* kutoka Iringa hadi Shinyanga.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** Fedha zinazohitajika kutekeleza Mradi huu kwa Miaka Mitano ni takriban **Shilingi trilioni 7**. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali imetenga kiasi cha **Shilingi bilioni 469.09** fedha za Ndani na **Shilingi bilioni 30** fedha za Nje.

**(iii)** ***Mradi wa Mfano wa Kupunguza Gharama za Miundombinu ya Usambazaji Umeme Vijijini (Low Cost Design Standards for Rural Electrification)***

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kupunguza gharama za ujenzi wa miundombinu ya usambazaji umeme vijijini, Serikali ilipata ruzuku kutoka Benki ya Dunia ya kufanya utafiti kuhusu gharama

*Chanzo: REA, 2017*

hizi na kutekeleza Mradi wa Mfano. Utafiti huo ulifanyika katika Wilaya za Kilombero na Mbozi ambapo ulibaini kuwa gharama zinaweza kupungua kwa kati ya **asilimia 30** hadi **40** iwapo Miradi itatekelezwa kwa kutumia teknolojia ya gharama nafuu. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 kwenye Mradi huu kazi ya ujenzi wa miundombinu iliendelea na hadi kufikia Mwezi Desemba, 2016 kazi zilikuwa zimekamilika kwa **asilimia 96** (Mbozi) na **asilimia 94** (Kilombero). Mradi huu unatarajiwa kukamilika Mwezi Juni, 2017.

**(iv)** ***Utekelezaji wa Programu ya Awamu ya Pili ya Mradi wa Sustainable Solar Market Package (SSMP – II)***

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Programu ya Awamu ya Pili ya **Mradi wa Sustainable Solar Market Package (SSMP – II)** unahusu ujenzi wa Mifumo ya Umeme Jua katika Wilaya nane (8) za Biharamulo, Bukombe, Chato, Kasulu, Kibondo, Namtumbo, Sikonge na Tunduru. Hadi kufikia Mwezi Desemba, 2016, Jumla ya Mifumo Midogo ya Umeme 4,620 yenye

uwezo wa kWp 115 ilifungwa. Gharama za Mradi ni **Dola za Marekani milioni 18** sawa na **Shilingi bilioni 41.60** ambazo ni Mkopo kutoka Benki ya Dunia.

### (v) *Mradi wa Kuhamasisha Upelekaji na Matumizi ya Umeme Vijijini (Lighting Rural Tanzania) 2014*

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu ulihusisha kusambaza umeme unaotokana na Mifumo ya Nishati Jadidifu *(renewable energies)* kwa kujenga Gridi Ndogo Ndogo zinazojitegemea kwenye maeneo yaliyo mbali na Gridi ya Taifa na maeneo ya Visiwani. Mradi huu ulitekelezwa na Waendelezaji 18 kwa ujumla katika maeneo mbalimbali nchini. Mradi huu unatekelezwa katika maeneo ya vijijini katika Mikoa ya Arusha, Iringa, Kigoma, Lindi, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Njombe, Pwani, Ruvuma na Singida. Hadi kufikia Mwezi Desemba, 2016 Mradi ulikuwa umefikia **asilimia 72** na gharama za Mradi ni **Shilingi bilioni 4.** Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

*Chanzo: REA, 2017*

## *SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA*

### *Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia*

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2016/17 utafiti wa Mafuta na Gesi Asilia umeendelea kufanyika katika maeneo ya baharini na nchi kavu. Aidha, kushuka kwa bei za Mafuta na Gesi Asilia katika Soko la Dunia, kumeathiri kasi ya shughuli za utafutaji Mafuta na Gesi Asilia nchini. Pamoja na changamoto hizo, Jumla ya visima vitatu (3) vilichorongwa. Visima viwili (Kitatange-1 na Bunju-1) vilichorongwa na Kampuni ya Shell/BG katika Vitalu namba 1 na 4 vilivyopo kwenye kina kirefu cha maji ya Bahari ya Hindi ambapo vyote havikuwa na mashapo ya Gesi Asilia kama ilivyotarajiwa. Kisima cha tatu (Ntorya -2) kilichorogwa na Kampuni ya Ndovu Resources katika Kitalu cha Mtwara kuhakiki Gesi Asilia iliyogunduliwa katika Kisima cha Ntorya –1 na kazi ya kutathmini kiasi kilichopo inaendelea. Kwa sasa kiasi cha Gesi Asilia kilichogunduliwa nchini ni Jumla ya Futi za Ujazo (TCF) Trilioni 57.25 ambapo Gesi Asilia iliyogunduliwa Nchi

*Chanzo: REA, 2017*

Kavu ni TCF Trilioni 10.12 na kina kirefu cha Bahari ya Hindi TCF Trilioni 47.13. Hata hivyo, ugunduzi huu mpya uliofanywa katika Kisima cha Ntorya - 2 utaongeza kiasi cha Gesi Asilia iliyogunduliwa nchini baada ya tathmini kukamilika.

### *Matumizi ya Gesi Asilia Viwandani*

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jumla ya Viwanda 42 tayari vimeunganishwa na miundombinu ya Gesi Asilia. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Serikali kupitia TPDC imeendelea kutafuta Wateja wapya na kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya kusambaza Gesi Asilia. Majadiliano kati ya TPDC na Dangote Cement Tanzania Limited – Mtwara yamekamilika na majadiliano yanaendelea kati yake na Bakhressa Food Factory, Knauf Gypsum na Lodhia Steel vilivyopo Mkuranga Mkoani Pwani. Aidha, Kiwanda cha Goodwill Ceramic Tanzania Limited tayari kimeunganishwa na kuanza kutumia Gesi Asilia ambapo kitatumia Jumla ya Futi za Ujazo milioni saba kwa siku (7 mmscfd).

*Chanzo: REA, 2017*

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC itakamilisha mazungumzo na Kiwanda cha kuzalisha Mbolea cha Kilwa Masoko ambacho TPDC ni Mbia pamoja na Kampuni ya *Ferrostaal Industry Project GmbH* ya Ujerumani na Wabia wake *Holdor Topsoe A/S* na *Fauji Fertiliser Company Limited*. Kiwanda hiki hadi kukamilika kitagharimu kiasi cha **Dola za Marekani bilioni 1.92** sawa na takriban **Shilingi trilioni 4.44**. Mahitaji ya Gesi Asilia yanatarajiwa kuwa Futi za Ujazo milioni 104 kwa siku *(104 mmscfd)* na kitazalisha mbolea aina ya amonia tani 2,200 kwa siku pamoja na aina ya urea tani 3,850 kwa siku.

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, mawasiliano na Majadiliano kuhusu upatikanaji wa Gesi Asilia kwa Kiwanda cha kuzalisha Mbolea cha Mtwara chini ya Kampuni ya *Helm* ya Ujerumani na Wabia wake ambao ni Halmashauri za Mkoa wa Mtwara yanaendelea. Kiwanda hiki hadi kukamilika kitagharimu kiasi cha **Dola za Marekani bilioni 1.2** sawa na takriban **Shilingi trilioni 2.77**. Mahitaji ya Gesi Asilia yanatarajiwa kuwa Futi za Ujazo milioni 80 kwa siku (80 mmscfd) na kitazalisha mbolea tani 3,700 kwa siku.

*Chanzo: REA, 2017*

***Mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (Bulk Procurement System)***

**93. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea na usimamizi wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja kupitia Wakala wake *(Petroleum Bulk Procurement Agency – PBPA)*. Taratibu za uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja zimeainishwa katika Sheria ya Petroli *(The Petroleum Act, No. 21)* ya Mwaka 2015 pamoja na Kanuni za Uagizaji wa Bidhaa za Petroli kwa Pamoja - *(The Petroleum (Bulk Procurement) Regulations, 2017, GN No. 198 of 2017)*. Mfumo huu unaweka utaratibu wa mafuta yote kuagizwa kwa pamoja kwa kutumia utaratibu maalum unaowekwa ili pia kupata manufaa ya kiuchumi *(economies of scale)* na mafuta yanayokidhi ubora. Aidha, Mfumo huu umelenga kuhakikisha usalama wa upatikanaji wa mafuta *(security of supply of petroleum products)* nchini kwa wakati wote.

**94. *Mheshimiwa Spika,*** Mfumo wa zabuni ndio umekuwa unatumika katika kupata Kampuni zitakazoagiza na kuleta mafuta nchini. Kampuni za mafuta huwasilisha kwa Wakala kiasi cha mafuta ya

*Chanzo: REA 2017*

petroli, dizeli, mafuta ya ndege na mafuta ya taa wanachohitaji kuuza kwa Mwezi mzima. Baada ya kupata kiasi cha mafuta kutoka kwa Kampuni hizo, Wakala huandaa nyaraka za zabuni na baadaye kutoa taarifa ya zabuni hiyo kwa Kampuni zote zilizoidhinishwa *(pre-qualified)* kushiriki katika zabuni za kuleta mafuta. Mafuta yanayotakiwa kutumika hapa nchini ni lazima yaagizwe kwa kutumia Mfumo huu *(mandatory for locally used fuel),* lakini mafuta yanayopitia hapa nchini *(transit)* si lazima kuagizwa kwa kupitia Mfumo huu *(it is optional).*

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfumo huu umeleta mafanikio makubwa katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Taifa kwa ujumla. Baadhi ya mafanikio hayo ni kushuka kwa gharama ya manunuzi (*Premium*) kutoka wastani wa Dola za Marekani 50 kwa tani kabla ya utaratibu huu mpaka wastani wa takriban Dola za Marekani 20 kwa tani na uhakika wa usalama wa upatikanaji wa mafuta nchini. Hii ni kutokana na ukweli kwamba zabuni za mafuta ya Mwezi hutolewa zaidi ya Mwezi mmoja kabla ya muda husika, pamoja na uhakika wa usahihi wa takwimu

*Chanzo: REA, 2017*

za mafuta yaliyoagizwa na kuingia hapa nchini. Kutokana na takwimu hizi vyombo mbalimbali vinaweza kupanga mipango yake kwa ufanisi zaidi ikiwemo Mapato ya Serikali yatokanayo na Kodi za mafuta na kiasi cha fedha zinazoweza kupatikana kwa Mwezi kutokana na mafuta kwa ajili ya Mfuko wa Nishati Vijijini, Mfuko wa Barabara, n.k.

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfumo huu pia umesaidia kupunguza gharama za meli kusubiri kupakua mafuta *(Demurrage costs).* Hivi sasa gharama hizo ni kati ya **Dola za Marekani 1.6** na **3.5** kwa tani moja ya uzito tofauti na **Dola za Marekani 45** hadi **50** kwa tani moja ya uzito iliyokuwa kabla ya Mfumo huu kuanza kutumiwa. Kupungua kwa gharama hizi kunatokana na upangaji mzuri wa meli unaofanywa na PBPA na kuongezeka kwa sehemu za kupakulia mafuta. Jitihada za TPA kujenga sehemu ya SPM ambapo meli kubwa za dizeli zinaweza kupakua mafuta na vilevile kuanza kutumika kwa Bandari ya Tanga kumepunguza sana msongamano wa meli katika sehemu ya Kurasini *Oil Jet One (KOJ 1).*

*Chanzo: REA, 2017*

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Mfumo huu umewezesha EWURA kupanga bei elekezi kwa kutumia takwimu sahihi za bei ya Mafuta katika Soko la Dunia na gharama za kusafirisha mafuta hadi hapa nchini. Aidha, Mfumo huu umepunguza gharama za meli kusubiri kabla ya kupakua mafuta *(demurrage)* na umewezesha kudhibiti ubora wa mafuta yanayoagizwa nchini.

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwezi Januari hadi Desemba, 2016 Jumla ya **lita bilioni 4.97** za mafuta ziliingizwa nchini ambapo **lita bilioni 4.73** ziliingizwa kupitia Bandari ya Dar es Salaam na **lita milioni 237.85** ziliingizwa kupitia Bandari ya Tanga. Kati ya mafuta hayo, **lita bilioni 2.34** sawa na **asilimia 47.11** yalikuwa kwa ajili ya matumizi ya ndani na lita **bilioni 2.65** sawa na **asilimia 52.89** yalikuwa kwa ajili ya Nchi Jirani.

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafuta kwa ajili ya matumizi ya ndani yameongezeka kwa **asilimia 2.23** kutoka **lita bilioni 2.29** Mwaka 2015 hadi **lita bilioni 2.34** Mwaka 2016. Aidha, mafuta yaliyoagizwa kwa ajili ya

Nchi Jirani (Burundi, DRC, Rwanda, Uganda na Zambia) yameongezeka kwa **asilimia 3.02** kutoka **lita bilioni 2.57** Mwaka 2015 hadi **lita bilioni 2.65** Mwaka 2016. Ongezeko hilo linatokana na kukua kwa mahitaji ya mafuta ndani ya nchi hizo pamoja na nchi jirani kuongeza uagizaji wa mafuta kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali itaanzisha Mpango wa kuongeza upakuaji wa mafuta kwa kutumia Bandari ya Tanga yatakayokuwa yanasambazwa Mikoa ya Kaskazini mwa nchi na pia kuanzisha Mfumo huu kwa Bandari ya Mtwara kwa kusambaza katika Mikoa ya Kusini mwa nchi na Nchi Jirani. Vilevile, kuanzisha uingizaji wa bidhaa za *Liquified Petroleum Gas (LPG)* kwa kutumia Mfumo kama huu ili kuweza kupata faida zinazopatikana kwa Mfumo wa uagizaji kwa pamoja.

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** uagizaji wa mafuta kwa pamoja umeendana na uboreshaji wa viwango vya mafuta anayonunua mlaji wa mwisho katika kituo. Ili

*Chanzo: REA, 2017*

kudhibiti ubora wa mafuta, Serikali ilifanya uamuzi wa kupunguza tofauti kati ya bei ya Mafuta ya Taa na bei ya mafuta ya Petroli na Dizeli. Kuimarisha udhibiti wa ubora wa mafuta, vinasaba vimekuwa vikitumika kubaini uchanganyaji wa mafuta unaoathiri ubora. Hata hivyo, utaratibu wa matumizi ya vinasaba umekuwa ukilalamikiwa na baadhi ya wadau hali iliyosukuma Wizara yetu kuangalia kwa makini mfumo huu mwaka wa fedha ujao.

***Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia (LNG Project)***

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 taarifa ya tathmini ya athari za mazingira na kijamii imekamilika. Pamoja na taarifa hiyo, Mpango wa kuwapatia maeneo mbadala Wananchi waishio katika eneo litakalojengwa Mitambo ya LNG la Likong’o Mkoani Lindi *(Ressettlement Action Plan)* umekamilika. Vilevile, kazi za kuingiza Michoro ya eneo la Mradi wa LNG kwenye Ramani ya Mipango Miji imekamilika. Aidha, utaratibu wa

*Chanzo: REA, 2017*

uvunaji Gesi Asilia kutoka kina kirefu cha maji ya Bahari ya Hindi hadi eneo la nchi kavu *(Concept selection)* kwa Kitalu Na.1 na Kitalu Na.2 umekamilika na kwa Kitalu Na.4 unatarajiwa kukamilika katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18.

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** Majadiliano ya kufikia Makubaliano ya utekelezaji wa Mradi *(Host Government Agreement - HGA)* kati ya Kikosi Kazi cha Wataalam wa Serikali *(Government Negotiation Team)* na Kampuni za Utafutaji Mafuta na Gesi Asilia (IOCs) yalianza rasmi Mwezi Septemba, 2016. Mradi huu utachukua muda wa takribani Miaka nane (8) hadi kumi (10) kufikia uzalishaji na utagharimu takriban **Dola za Marekani bilioni 30**, sawa na takriban **Shilingi trilioni 69.33**. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 **Shilingi bilioni 13** zimetengwa kwa ajili ya malipo ya fidia, upatikanaji wa ardhi pamoja na shughuli nyingine za Mradi huu.

*Chanzo: REA, 2017*

## *Miradi ya Usafirishaji wa Mafuta na Gesi Asilia*

### *Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kutoka Kabaale (Uganda) hadi Bandari ya Tanga (Tanzania)*

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kushiriki kwa karibu katika matayarisho ya ujenzi wa Bomba la kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Kabaale (Uganda) hadi Tanga (Tanzania), kilomita 1,445. Kazi zilizofanyika hadi Mwezi Machi, 2017 ni pamoja na: kusainiwa kwa Mkataba wa Makubaliano ya Awali *(MoU);* kutolewa kwa Vivutio vya Kodi; kufanya tathmini ya njia ya Bomba *(survey)*; tathmini ya mahitaji ya njia ya Bomba *(infrastructure requirements)*; na Tathmini ya Athari ya Mazingira Kijamii *(Environmental and Social Impact Assesment)* na kusainiwa kwa *Inter-Governmental Agreement (IGA)* tarehe 26 Mei, 2017. Gharama za Mradi huu ni **Dola za Marekani bilioni 3.5** sawa na takriban **Shilingi trilioni 8.09**. Wadau Wakuu katika Mradi huu ni Kampuni ya TOTAL (Ufaransa),

*Chanzo: REA 2017*

CNOOC (China) na TULLOW (Uingereza) pamoja na Serikali za Tanzania na Uganda.

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 ni pamoja na Mabunge ya nchi husika (Tanzania na Uganda) kuridhia Mkataba huo; kuanza Mazungumzo ya Mkataba baina ya Serikali husika na Kampuni ya Bomba *(Host Government Agreement - HGA)*; kuanza Mazungumzo ya Mkataba wa Wanahisa *(Shareholders Agreement)*; kuanza Mazungumzo ya Mkataba baina ya Mamlaka ya Bandari (TPA) na Kampuni ya Bomba; Mwekezaji kukamilisha usanifu wa Mradi *(Front End Engineering Design - FEED)*, upimaji *(survey)* wa eneo la kujenga ghala katika Bandari ya Tanga; utafiti katika Mkuza wa Bomba na katika eneo la Bahari karibu na Bandari ya Tanga *(mateocean and geophysical technical studies)*.

*Chanzo: REA, 2017*

### *Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Safi (White Petroleum Products) kutoka Dar es Salaam (Tanzania) hadi Ndola (Zambia)*

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Safi *(White Petroleum Products)* kutoka Dar es Salaam (Tanzania) hadi Ndola (Zambia) unahusisha ujenzi wa Bomba lenye urefu wa takriban kilomita 1,710 litakalojengwa sambamba na Bomba la TAZAMA linalosafirisha Mafuta Ghafi *(Crude Oil)* kutoka Dar es Salaam hadi Ndola. Bomba Jipya litakuwa na uwezo wa kusafirisha tani milioni nne (4) za mafuta kwa Mwaka. Mradi huu pia utahusisha ujenzi wa Mabomba ya Matoleo ya mafuta *(take-off points)* katika maeneo ya Morogoro, Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe. Gharama za Mradi huu zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani bilioni 1.5** sawa na **Shilingi trilioni 3.47**.

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** Makubaliano ya kuanza ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Safi yalitokana na ziara ya Rais wa Jamhuri ya Zambia **Mhe. Edgar Chagwa**

**Lungu,** aliyoifanya nchini Tanzania tarehe **29 Novemba, 2016** na kukutana na Mwenyeji wake Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.** Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi huu ni kuunda Kamati Ndogo *(sub - committees)* chini ya Makatibu Wakuu wanaoshughulikia masuala ya Nishati zitakazojadili masuala ya Sheria *(Legal and Institutional framework),* Fedha *(Fiscal and Financing Options)* na Utaalam *(Technical Issues);* kuandaa Andiko la Mradi *(Project Concept Paper)*; kutengeneza Hadidu za Rejea *(Terms of Reference)* kwa ajili ya kufanya Upembuzi Yakinifu *(Feasibility Study)* utakaoonesha gharama za Mradi na namna bora ya kutekeleza Mradi. Kazi nyingine inayoendelea ni kupitia Mikataba iliyopo ya Kisheria na ya Kifedha ya TAZAMA *(TAZAMA Convention, 1968, Article of Association of TAZAMA).*

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa Bomba hili utafanywa kwa ushirikiano wa nchi mbili za Tanzania na Zambia na utaleta manufaa makubwa kwa nchi zote. Kwa upande wa Tanzania manufaa

*Chanzo: REA, 2017*

yatakayopatikana ni pamoja na uhakika wa upatikanaji wa mafuta nchini hususan Mikoa ya Dodoma, Iringa, Katavi, Mbeya, Morogoro, Njombe, Ruvuma, Shinyanga, Singida, Songwe, Rukwa na Tabora; ufanisi, usalama na bei nafuu katika kusafirisha mafuta ikiwa ni pamoja na kupunguza matumizi ya malori ya mafuta ambayo yamekuwa yakiharibu miundombinu ya barabara. Utekelezaji wa Mradi huu unatarajiwa kuanza Mwaka 2018 na kukamilika Mwaka 2021.

***Miradi ya Usambazaji Gesi Asilia Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara na Pwani***

**109. *Mheshimiwa Spika,*** Mwezi Desemba, 2016 Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) lilitangaza zabuni ya kumpata Mshauri Mwelekezi ili kuhuisha taarifa ya Upembuzi Yakinifu na usanifu wa kina wa michoro ya Mradi wa Kusambaza Gesi Asilia Mkoani Dar es Salaam. Utaratibu wa kukamilisha zoezi la kumpata Mshauri linatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Mwezi Juni, 2017. Taarifa ya Mshauri itakayopatikana itatumika kushawishi Taasisi za Fedha zilizoonesha nia ya kufadhili

*Chanzo: REA 2017*

Mradi huu zikiwemo, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Benki ya Exim ya China. Katika Mwaka wa Fedha 2017/18 Serikali imetenga **Shilingi bilioni 1** kwa ajili ya uhuishaji wa taarifa ya Upembuzi Yakinifu. Aidha, kwa upande wa Mikoa ya Pwani, Lindi na Mtwara, Serikali kupitia TPDC imeendelea na juhudi za kutafuta fedha za Mikopo ya riba nafuu kwa ajili ya utekelezaji wa usambazaji Gesi Asilia kwa ajili ya matumizi ya viwandani, majumbani na Taasisi mbalimbali kwenye Mikoa hiyo.

## *SEKTA NDOGO YA NISHATI JADIDIFU*

### *(i) Nishati ya Jua (Solar Energy)*

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi ilifanikisha kupatikana kwa **MW 1** katika maeneo ambayo yako nje ya Gridi ya Taifa kwenye Kisiwa Cha Bwisya kilichopo Ziwa Viktoria na maeneo mengine katika Wilaya za Simanjiro Mkoani Manyara na Lumuli Mkoani Iringa. Aidha, kupitia Mfumo wa Usambazaji wa Umeme wa Jua Majumbani na kwenye Taasisi

*Chanzo: REA 2017*

za Afya na Elimu *(Solar Home Systems),* kiasi cha **MW 2** kilipatikana katika maeneo mbalimbali nchini na kufanya upatikanaji wa umeme kwa kupitia Mfumo huu kufikia takriban **MW 9**.

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali itakamilisha uandaaji wa Ramani ya maeneo yenye fursa za uwekezaji wa uzalishaji wa umeme wa Jua ikijumuisha uainishaji wa miundombinu husika kwa lengo la kuvutia uwekezaji katika Sekta Ndogo hii. Aidha, Serikali kupitia TANESCO itaanza kufanya Upembuzi Yakinifu katika Maeneo ya Kishapu na Visiwa vya Mafia kwa ajili ya uzalishaji umeme wa Jua kwa kati ya **MW 50** hadi **300**. Serikali pia kwa kushirikiana na Sekta Binafsi itahakikisha kuwa Visiwa zaidi vya Ziwa Victoria vikiwemo vya Bukerebe, Bulubi, Bushengele, Bwiro, Izinga, Kamasi, Kweru Kuu, Kweru Mto, Sizu na Zeru vinapatiwa umeme kupitia Gridi Ndogo za Umeme wa Jua. Aidha, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Wasambazaji wa vifaa na Mifumo ya Umeme Jua ili maeneo mengine yaliyo pembezoni yapate umeme kwa njia hii.

*Chanzo: REA, 2017*

## *(ii) Nishati ya Upepo (Wind Energy)*

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** uwekezaji katika Nishati ya Upepo kwa kiasi kikubwa unaathiriwa na upatikanaji wa ardhi. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Serikali kwa kushirikana na Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe na Halmashauri ya Mji wa Makambako ilifanya utatuzi wa mgogoro wa ardhi kati ya Mwekezaji (Kampuni ya Sino-Tan) na Halmashauri husika. Kazi inayoendelea ni kupitia upya tathmini ya fidia kwa wananchi watakaopisha utekelezaji wa Mradi. Aidha, Kampuni ya Windlab ya Afrika Kusini ilianza utafiti wa takwimu za Upepo ili kuwekeza katika eneo la Makambako. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali itafanya tathmini ya kina na ufuatiliaji wa Miradi ya Umeme wa Upepo na kuwabaini Waendelezaji wanaohodhi maeneo kwa muda mrefu bila kuyaendeleza ili maeneo hayo yaweze kushindanishwa na kupewa Waendelezaji wenye uwezo wa kuyaendeleza. Kiasi cha **Shilingi bilioni 1.3** ambazo ni fedha za Nje kimetengwa kwa ajili ya uendelezaji wa Miradi ya Nishati ya Jua na Upepo.

*Chanzo: REA, 2017*

### *(iii) Miradi ya Tungamotaka (Bio- Energies)*

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 uzalishaji wa umeme kwa kutumia Tungamotaka *(Biomass)* zitokanazo na mabaki ya miwa katika Viwanda vya Sukari, mazao ya misitu na mkonge umefikia **MW 38** ambapo **MW 10.5** zimeunganishwa kwenye Gridi ya Taifa na **MW 27.5** zinatumika kwa ajili ya shughuli za Viwanda husika. Viwanda hivyo ni Tanganyika Planting Company (TPC) cha Mkoani Kilimanjaro **MW 10**; Kilombero Sugar Company Limited cha Mkoani Morogoro **MW 9**; Mtibwa Sugar cha Mkoani Morogoro **MW 5**; Kagera Sugar cha Mkoani Kagera **MW 5**; Tanzania Wattle Company (TANWAT) cha Mkoani Iringa **MW 2.5**; Ngombeni Biomass Project cha Mafia **MW 1** na Mkonge Energy cha Mkoani Tanga **MW 1**. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Wizara itaendelea na uhamasishaji wa Sekta Binafsi ili kuongeza uzalishaji wa umeme utokanao na Tungamotaka. Hatua hii itaongeza mchango wa Tungamotaka katika upatikanaji wa umeme nchini kwa takriban **MW 2** ambazo

*Chanzo: REA 2017*

zitaongezwa kwenye Gridi ya Taifa na kiasi kingine zaidi kutumika kwa ajili ya Viwanda husika.

### *(iv) Miradi ya Jotoardhi (Geothermal)*

**114. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi *(Tanzania Geothermal Development Company Limited - TGDC),* ambayo ni Kampuni Tanzu ya TANESCO, imekamilisha utafiti wa kina *(detail surface study)* wa uendelezaji Nishati ya Jotordhi katika maeneo ya Ziwa Ngozi (Mbeya) mnamo Mwezi Septemba, 2016, chini ya ufadhili wa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP) na Shirika la Maendeleo la Iceland (ICEIDA). Aidha, utafiti umeweza kuainisha sehemu tatu (3) za kuchoronga Visima vya Majaribio (*Slim Wells*) katika eneo la Ziwa Ngozi ili kutathmini kiasi cha hifadhi ya rasilimali ya Jotoardhi na uwezo wake wa kuzalisha umeme. Vilevile, Serikali kupitia Mshauri Mwelekezi ambaye ni Electro-consult ya nchini Italia chini ya ufadhili wa Serikali ya Iceland kupitia Shirika la

*Chanzo: REA, 2017*

Maendeleo la Iceland (ICEIDA) yupo katika hatua za mwisho za kukamilisha utafiti wa kina (*detail surface studies*) katika maeneo ya Mbaka-Kiejo, Mkoani Mbeya na Luhoi Mkoani Pwani.

**115. *Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Serikali kupitia TGDC imejipanga kutekeleza Mradi wa uchorongaji Visima Vitatu (3) vya utafiti katika eneo la Ziwa Ngozi. Gharama za Mradi ni **Dola za Marekani milioni 12** sawa na **Shilingi bilioni 27.73**. Mradi huu utafadhiliwa na Serikali kwa kushirikana na Mfuko wa Uendelezaji Jotoardhi *(Geothermal Risk Mitigation Facility - GRMF)* ulio chini ya Kamisheni ya Afrika (AUC). Serikali itagharamia kiasi cha **Dola za Marekani milioni 8.78** sawa na **Shilingi bilioni 20.29** na kiasi kilichobakia cha **Dola za Marekani milioni 3.33** sawa na **Shilingi bilioni 7.70** kitatolewa na GRMF kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18.

*Chanzo: REA, 2017*

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Serikali kupitia TGDC inategemea kufanya utafiti wa kina *(detail surface study)* katika eneo la Kisaki, Mkoani Morogoro kwa kushirikiana na GRMF. Gharama za Mradi huu ni kiasi cha **Dola za Marekani milioni 1.32** sawa na **Shilingi bilioni 3.05**. Serikali itachangia kiasi cha **Dola za Marekani 165,210** sawa na **Shilingi milioni 381.80** na GRMF itachangia kiasi cha **Dola za Marekani milioni 1.16** sawa na **Shilingi bilioni 2.68.**

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TGDC inaendelea kutathmini uendelezaji wa rasilimali ya Jotoardhi kwa ajili ya matumizi ya moja kwa moja *(direct heat uses)*. Matumizi hayo ni pamoja na kutengeneza mabwawa ya kuogelea ya maji moto pamoja na uboreshaji wa sehemu hizo za asili ambazo huvutia utalii. Matumizi mengine ni pamoja na uzalishaji wa mazao ya kilimo cha maua na mboga mboga, ukaushaji wa nafaka, ufugaji wa samaki na shughuli za viwandani *(industrial processes)*. Miongoni mwa sehemu ambazo zinaweza kuendelezwa kwa matumizi hayo ni Ibadakuli iliyoko

*Chanzo: REA, 2017*

Mkoani Shinyanga na Songwe katika Mkoa wa Songwe.

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwa na uendelezaji endelevu wa Nishati ya Jotoardhi nchini, Serikali inaendelea na uandaaji wa Mpango Mkakati wa Uendelezaji wa Jotoardhi na Sheria ya kuendeleza Jotoardhi nchini. Mpango wa kumpata Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kazi hii utakamilika Mwezi Agosti, 2017. Utekelezaji wa kazi hizi unafadhiliwa na *Climate Investment Funds (CIF)* kupitia Mpango wa *Scaling Up Renewable Energy Programme(SREP)* kupitia Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa gharama ya **Dola za Marekani 450,000,** sawa na takriban **Shilingi milioni 1.04**.

### *(v) Umeme wa Maporomoko Madogo ya Maji (Mini-Hydro)*

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuhamasisha uendelezaji wa Miradi ya Maporomoko Madogo ya Maji ili kuhakikisha inatoa mchango katika kuwafikishia umeme Wananchi na hasa wa vijijini. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17

*Chanzo: REA, 2017*

kiasi cha **MW 36.99** kutoka Maporomoko Madogo ya Maji kilizalishwa ambapo **MW 6.11** zimeunganishwa kwenye Gridi ya Taifa na kiasi cha **MW 30.88** kinatumika katika Gridi Ndogo Ndogo na Taasisi. Baadhi ya maeneo hayo yenye Maporomoko Madogo ya Maji ni Andoya (Mbinga), Darakuta (Manyara), Ikondo (Njombe), Kiliflower (Arusha), Mwenga (Mufindi), Tulila (Songea) na Yovi (Kilosa).

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali itaendelea kuhamasisha uendelezaji wa Miradi ya Maporomoko Madogo ya Maji ili kuhakikisha inatoa mchango wa upatikanaji wa umeme wa bei nafuu nchini.

### *(vi) Usambazaji Umeme kwa Mfumo wa Gridi Ndogo (Mini-Grids)*

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Serikali ilifanya ukaguzi na uhakiki wa Mifumo ya Gridi Ndogo ili kubaini changamoto zinazowakabili Waendelezaji. Katika kutatua changamoto hizo, Serikali iliandaa Viwango na Kanuni za usimamizi wa Gridi Ndogo

*Chanzo: REA, 2017*

zinazotoa Mwongozo wa uendeshaji wake hususan pale eneo husika linapofikiwa na Gridi ya Taifa. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali itaendelea kuweka mazingira bora ya uendelezaji wa Gridi Ndogo za Umeme ili kuwezesha Wananchi kupata umeme hasa maeneo ya Visiwa na yale yaliyo pembezoni. Aidha, kupitia REA III, Mradi huu umetengewa **Shilingi bilioni 50** ambazo ni fedha za Nje kutoka Serikali za Uingereza na Sweden ambapo Jumla ya **MW 26.9** zinatarajiwa kuzalishwa.

### *(vii) Uendelezaji wa Matumizi ya Bayogesi (Biogas)*

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Serikali kwa kushirikiana na Kituo cha Usambazaji na Uendelezaji wa Teknolojia ya Kilimo Vijijini *(Center for Agricultural Mechanization and Rural Technology* - CAMARTEC*)* imewezesha ujenzi wa Mitambo 1,980 na kufanya Jumla ya idadi ya Mitambo iliyojengwa kufikia 15,980 tangu Programu ianze Mwaka 2009. Wananchi 95,880 katika Mikoa yote ya

*Chanzo: REA, 2017*

Tanzania Bara walinufaika na programu hii kwa kuweza kumiliki Mitambo na kutumia Bayogesi kwa ajili ya kupikia na kuwasha taa. Aidha, Makampuni Binafsi ya ujenzi wa Mitambo ya Bayogesi yapatayo 100 yalianzishwa na kutoa ajira kwa Watanzania takriban 1,000. Ili kuongeza msukumo wa ujenzi wa Mitambo mingi ya Bayogesi nchini, Mwaka 2016 Serikali kupitia Mfuko wa Nishati Vijijini ilianza kutoa ruzuku kwa ajili ya ujenzi wa Mitambo 10,000 nchini. Gharama ya Utekelezaji wa Progamu nzima hadi kufikia Mwaka 2019 ni **Dola za Marekani milioni 10.7** sawa na takriban **Shilingi bilioni 24.73**. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Jumla ya **Shilingi bilioni 1.5** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza Mradi huu.

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali itaendelea kutoa ruzuku kupitia Mfuko wa Nishati Vijijini ili kuhamasisha Kampuni za uzalishaji mkonge, korosho pamoja na Halmashauri za Miji kutumia teknolojia ya Bayogesi katika uzalishaji wa umeme kwa lengo la kuongeza thamani ya mazao na

*Chanzo: REA, 2017*

utunzaji wa mazingira kwa kutumia Mabaki ya Mazao na Taka za Mijini. Kupitia Mpango huu, REA imetenga Jumla ya **Shilingi bilioni 50** kwa ajili ya kutekeleza Miradi mbalimbali ya Nishati Jadidifu ikiwemo teknolojia ya Bayogesi.

### ***(viii) Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Upatikanaji wa Nishati Endelevu kwa Wote (Sustainable Energy for All initiative - SE4ALL)***

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania ni moja ya nchi zinazotekeleza Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Nishati Endelevu unaojulikana kama *Sustainable Energy for All* (SE4ALL). Mpango huu una lengo la kuwapatia nishati bora watu wote Duniani ifikapo Mwaka 2030. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Wizara ilikamilisha maandalizi ya "*Action Agenda*" na "*Investment Prospectus*" ambazo ni Miongozo muhimu katika utekelezaji wa malengo ya SE4All. Aidha, Serikali kupitia ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ilianza maandalizi ya kuandaa utaratibu wa utekelezaji wa miongozo hii. Vilevile, kupitia ufadhili wa

*Chanzo: REA, 2017*

Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Wizara ilikamilisha maandalizi ya Programu ya Miaka Mitano (5) ambayo itasaidia kuanza kwa utekelelezaji wa Mpango wa SE4ALL.

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua mchango wa Tanzania katika jitihada zake za utekelezaji wa SE4ALL, Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Umoja wa Mataifa uliichagua Tanzania kuwa Mwenyeji wa Mkutano wa SE4ALL kwa nchi za Afrika zinazoendelea uliofanyika tarehe 5 hadi 6 Desemba, 2016. Mkutano huo uliandaliwa kwa ushirikiano na Ofisi ya Umoja wa Mataifa (UN) inayoshughulikia nchi zinazoendelea *(Office of the High Representative for LCDS)* pamoja na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP).

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali kwa kushirikiana na UNDP, AfDB na Wadau wengine wakiwemo Umoja wa Ulaya na Benki ya Dunia itaendelea na utekelezaji wa SE4ALL ikiwa ni pamoja na uhamasishaji wa

*Chanzo: REA, 2017*

upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi iliyobainishwa katika Mpango wa Uwekezaji wa SE4ALL *(Investment Prospectus)* na uratibu wa shughuli za Programu hii.

### *(ix) Mpango wa Matumizi Bora ya Nishati (Energy Efficiency)*

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** Matumizi Bora ya Nishati *(Energy Efficiency)* ni suala linalotakiwa kupewa kipaumbele ili kupunguza upotevu wa nishati kuanzia uzalishaji, usafirishaji, usambazaji hadi mtumiaji wa mwisho. Kutokana na juhudi mbalimbali zilizofanywa na Serikali pamoja na TANESCO zikiwemo za kukarabati na kuwekeza katika njia za usafirishaji na usambazaji wa umeme, upotevu wa umeme umepungua kutoka **asimilia 21** ya Mwaka wa Fedha wa 2015/16 hadi **asilimia 17** kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali itaendelea na uwekezaji wa kuboresha njia za usafirishaji na usambazaji umeme ili kuhakikisha kwamba upotevu wa umeme unashuka hadi kufikia **asilimia 16**.

*Chanzo: BEI, 2017*

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Watumiaji wa mwisho *(demand side)*, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Serikali kwa ufadhili wa Jumuiya ya Ulaya (EU) imeandaa Mpango Mkakati wa Matumizi Bora ya Nishati ulioweka mipango na Miradi mbalimbali ya kuzuia upotevu wa nishati katika nyumba za makazi, majengo ya biashara, viwanda na Taasisi. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali wakiwemo Umoja wa Ulaya (EU), Sida, NORAD na GIZ itaendelea kutekeleza Mradi huu.

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** Gharama za Nishati hususan umeme zinachukua sehemu kubwa ya gharama za uzalishaji katika viwanda. Ili kuongeza ushindani wa viwanda vyetu ni muhimu kupunguza gharama za uendeshaji kwa kudhibiti upotevu wa nishati na matumizi yasiyo ya lazima. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumani *(GIZ)* imeandaa Mpango Kazi wa Matumizi Bora ya Nishati kwa Watumiaji Wakubwa *(Energy Efficiency Action Plan for Designated Consumers)* na itatekeleza

*Chanzo: REA, 2017*

Mpango huo kwa kushirikiana na GIZ katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18. Mradi huu unakadiriwa kugharimu kiasi cha **Euro milioni 10** sawa na **Shilingi bilioni 21.3** na utatekelezwa katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2017/18 hadi 2020/21.

## SEKTA YA MADINI

### *Utafutaji na Ugunduzi Nchini wa Gesi ya Helium*

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuchukua hatua na kuweka mipango mbalimbali ya kuendeleza utafutaji na ugunduzi wa Gesi ya Helium ambayo ni adimu Duniani. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Kampuni ya Helium One Limited imeendelea kufanya utafiti wa Gesi hiyo kupitia Kampuni zake Tanzu za Gogota (TZ) Limited, Njozi (TZ) Limited na Stahamili (TZ) Limited zenye leseni za utafutaji katika maeneo mbalimbali ya Mikoa ya Rukwa na Manyara (Ziwa Eyasi na Balangida). Katika kutekeleza kazi hizo, Kampuni hiyo ilitoa Kandarasi kwa Vyuo Vikuu vya Oxford na Durham vya nchini Uingereza kufanya

*Chanzo: REA, 2017*

utafiti katika leseni zake zilizopo Ziwa Rukwa. Utafiti uliofanywa na Vyuo hivyo umewezesha kugundulika kwa Helium ya wingi wa takriban Futi za Ujazo bilioni 54 kutokana na sampuli za mavujia *(gas seeps)* zilizochukuliwa na kufanyiwa uchunguzi katika maeneo matano (5) yaliyopo eneo la Ziwa Rukwa. Kiasi hicho kinakadiriwa kuwa kikubwa zaidi ya mara sita (6) ya mahitaji ya Dunia kwa sasa.

**131. *Mheshimiwa Spika,*** Kazi ya uchorongaji wa Visima vya Utafiti katika maeneo hayo zinatarajiwa kuanza Mwaka 2018. Kazi hiyo itawezesha kuhakiki kiasi halisi cha Gesi ya Helium kilichopo katika maeneo ilipogunduliwa. Aidha, uchimbaji wa Gesi ya Helium utaanza mara baada ya kukamilika kwa kazi ya utafiti wa kina, Upembuzi Yakinifu na Tathmini ya Athari za Mazingira na pia leseni ya uchimbaji wa Gesi hiyo kutolewa. Kwa sasa shughuli za kukusanya taarifa zaidi za kijiolojia, kijiofizikia, na *2D Seismic survey* zinaendelea ili zitumike kwa ajili ya uchorongaji wa Visima vya Utafiti *(Exploration wells).* Gesi

*Chanzo: REA, 2017*

ya Helium, pamoja na matumizi mengine hutumika kupooza mashine za *MRI Scanners* na vinu vya *nuclear* na pia hutumika katika *floating balloons.* Serikali imeunda Kikosi Kazi chake ambacho kitafanya kazi na Wataalam Wazoefu  kutoka nchi zenye uzoefu mkubwa wa Gesi ya Helium.

***Ukusanyaji wa Mapato yatokanayo na Shughuli za Uchimbaji Madini Nchini***

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Wizara ilikusanya Mrabaha wa Jumla ya **Dola za Marekani milioni 56.77** sawa na takriban **Shilingi bilioni 131.20** kutoka kwenye Migodi Mikubwa ya Bulyanhulu, Buzwagi, Geita, NewLuika, North Mara, STAMIGOLD, TanzaniteOne, Mwadui, Ngaka na Dangote. Pia, kiasi cha Mrabaha wa **Shilingi bilioni 4.23** kilikusanywa kutokana na mauzo ya dhahabu iliyozalishwa kwa kuchenjua marudio kwa teknolojia ya *"vat leaching".* Aidha, Mrabaha wa **Shilingi bilioni 4.45** ulikusanywa kutokana na uzalishaji wa madini ya ujenzi na viwandani kutoka kwa Wachimbaji Wadogo. Makusanyo hayo

*Chanzo: REA, 2017*

yametokana na kazi ya ukaguzi na uhakiki wa madini yaliyozalishwa katika Migodi hiyo inayofanyika kwa ushirikiano baina ya Ofisi za Madini za Kanda na Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA). Vilevile, Wizara imekusanya kiasi cha **Shilingi milioni 14.52** kutokana na ada za Leseni na Vibali mbalimbali.

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Wizara ilikusanya Mrabaha wa **Dola za Marekani milioni 2.40** sawa na **Shilingi bilioni 5.55** kutokana na mauzo ya Almasi na **Dola za Marekani 906,347** sawa na **Shilingi bilioni 2.09** kutokana na mauzo ya vito ghafi na vilivyokatwa mathalan *Tanzanite, Garnet, Moonstones, Ruby, Spinel, Tourmaline, Garnet, Sapphire, Amethyst, Tsavorite* na *Zircon*. Malipo haya yalitokana na kazi ya uthamini iliyofanywa na *Tanzania Diamond Sorting Unit- TANSORT*.

*Chanzo: REA, 2017*

**134. *Mheshimiwa Spika,*** pamoja kupungua kwa shughuli za uwekezaji katika Sekta ya Madini katika miaka hivi karibuni kulikotokana na kushuka kwa bei ya madini katika soko la dunia, mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa umeongezeka kufikia Asilimia 4 Mwaka 2015 kutoka Asilimia 3.7 Mwaka 2014/15.

**135. *Mheshimiwa Spika,*** aidha, Ajira za moja kwa moja (*direct employment*) kwa Watanzania kwenye migodi mikubwa nchini imepungua kutoka 7,335 Mwaka 2015 na kufikia 6,207 mwaka 2016 ikiwa ni punguzo la Asilimia 15. Punguzo hilo limesababishwa na migodi kupunguza wafanyakazi hususan wa ajira za muda na mikataba kutokana na kushuka kwa bei ya dhahabu. Aidha, idadi ya wataalam toka nje ya nchi *(expatriates)* imepungua kutoka 333 mwaka 2015 na kuwa 294 mwaka 2016 ikiwa ni punguzo la Asilimia 12.

**136. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho hicho, Wizara kupitia TMAA ilifanya ukaguzi wa hesabu za Fedha za

*Chanzo: REA, 2017*

Migodi Mikubwa na ya kati kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kuiwezesha Serikali kukusanya Kodi ya Mapato *(Corporate Tax)* ya Jumla ya **Shilingi bilioni 79.26** kutoka kwa Kampuni za uchimbaji mkubwa wa dhahabu nchini. Kati ya malipo hayo, **Shilingi bilioni 45.76** zimelipwa na Kampuni ya Geita Gold Mining Limited na **Shilingi bilioni 33.50** zimelipwa na Kampuni ya North Mara Gold Mine Limited. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara kupitia Wakala wa Ukaguzi wa Madini (TMAA) itaendelea kufanya ukaguzi ili kuhakikisha malipo stahiki, hususan Kodi ya Mapato *(Corporate Income Tax)* yanalipwa Serikalini.

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Serikali inalenga kukusanya Jumla ya **Shilingi bilioni 194.4** katika Sekta ya Madini ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 215.96** zilizokadiriwa kukusanywa kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17. Kiasi hicho ni sawa na upungufu wa **asilimia 9.98**. Upungufu huo unatokana na kushuka kwa bei ya Dhahabu kwenye Soko la Dunia na kupungua kwa

*Chanzo: REA, 2017*

shughuli za utafutaji wa Madini nchini. Wizara itaendelea kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa shughuli za madini ikiwa ni pamoja na kuweka mkazo katika ukusanyaji wa ada na Mrabaha kutoka kwa Wachimbaji wa aina (kada) zote na Wafanyabiashara wa madini nchini ili kufikia lengo la ukusanyaji maduhuli kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18.

***Ushuru wa Huduma (Service Levy)***

**138. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi 2017, Kampuni za uchimbaji mkubwa wa madini zimeendelea kulipa Ushuru wa Huduma *(Service Levy)* kwa Halmashauri mbalimbali ambapo Jumla ya **Shilingi bilioni 11.27** zimelipwa. Kati ya Fedha hizo, Mgodi wa Geita umelipa kiasi cha **Shilingi bilioni 3.92** kwa Halmashauri ya Mji wa Geita; Mgodi wa Bulyanhulu **Shilingi milioni 760.57** kwa Halmashauriya WilayayaMsalala na **Shilingi milioni 374.61** kwa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'wale; Mgodi wa North Mara **Shilingi bilioni 3.10** kwa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime; Mgodi wa Buzwagi **Shilingi bilioni 1.48** kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama;

*Chanzo: RMA, 2017*

Mgodi wa New Luika **Shilingi milioni 697.77** kwa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya; na Mgodi wa STAMIGOLD **Shilingi milioni 167** kwa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo. Mgodi wa TanzaniteOne umelipa **Shilingi milioni 66** kwa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro; na Mgodi wa Wiliamson **Shilingi milioni 516.87** kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mwadui. Aidha, Kampuni ya Dangote Tanzania Limited imelipa **Shilingi milioni 187.92** kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara itaendelea kuzipatia Halmashauri husika takwimu sahihi za mauzo ya madini ili kuwezesha ukusanyaji wa ushuru wa Huduma kutoka kwa Kampuni zinazoendesha uchimbaji ndani ya Halmashauri zao.

***Uzalishaji na Mauzo ya Madini Nje ya Nchi***

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Jumla ya wakia milioni 1.05 za Dhahabu, wakia 414,128 za Fedha na ratili milioni 10.4 za Shaba zilizalishwa na kusafirishwa nje ya nchi kutoka Migodi Mikubwa ya

*Chanzo: REA, 2017*

STAMIGOLD, Bulyanhulu, Buzwagi, Geita, New Luika na North Mara. Thamani ya Madini yaliyosafirishwa kwa kila Mgodi ni kama ifuatavyo: Mgodi wa STAMIGOLD **Dola za Marekani milioni 15.09**, Mgodi wa Bulyanhulu **Dola za Marekani milioni 245.60**, Mgodi wa Buzwagi **Dola za Marekani milioni 174.35**, Mgodi wa Geita **Dola za Marekani milioni 465.76**, Mgodi wa New Luika **Dola za Marekani milioni 76.15** na Mgodi wa North Mara **Dola za Marekani milioni 381.02** ambapo Jumla ya thamani ya madini hayo ni **Dola za Marekani bilioni 1.36** sawa na **Shilingi trilioni 3.14.**

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho, Jumla ya karati 163,748 za Almasi na kilogram 2,872.79 za Tanzanite *(Grade A – I)* zilizalishwa na Migodi ya Mwadui na TanzaniteOne, sawia. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa shughuli za uzalishaji na biashara ya madini na kuwavutia Wawekezaji Wapya hususan kwenye madini ya *graphite* (kinywe), *lithium* na madini mengine yanayohitajika kwenye teknolojia ya kisasa *(Rare Earth Elements-*

*REE)* ili kuongeza mchango wa Sekta ya Madini katika maendeleo makubwa ya uchumi wa Taifa letu.

**141. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatambua umuhimu wa wawekezaji wakubwa wa nje na wa ndani katika uwekezaji kwenye Sekta ya Madini. Kwa Mwaka wa Fedha 2017/18, Serikali inadhamiria kwa kushirikiana na wadau kupitia Sera, Sheria na mikataba ya uendelezaji wa sekta hii ili kuhakikisha uwekezaji katika sekta unaendelea na kushimiri.

***Kuendeleza Shughuli za Uchimbaji Mdogo wa Madini***

**142. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na jitihada za kuendeleza uchimbaji mdogo wa madini nchini. Jitihada hizo ni pamoja na kutenga maeneo zaidi kwa ajili ya Wachimbaji Wadogo, kutenga Fedha zaidi za ruzuku na kuimarisha Shughuli za Ugani.

*Chanzo: REA, 2017*

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Wizara imetenga maeneo 11 kwa ajili ya Wachimbaji Wadogo wa madini yaliyopo Msasa na Matabe Mkoani Geita, Biharamulo na Kyerwa Mkoani Kagera, Itigi Mkoani Singida, D-Reef, Ibindi na Kapanda Mkoani Katavi, Ngapa Mkoani Ruvuma, Nzega Mkoani Tabora na Kitowelo Mkoani Lindi. Maeneo hayo yana ukubwa wa takriban **Hekta 38,951.7**. Aidha, Wizara kupitia Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST) inaendelea kufanya tathmini ya kina katika maeneo hayo ili kubaini uwepo wa mashapo ya madini zaidi kwa lengo la kuongeza tija kwa Wachimbaji Wadogo.

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwawezesha Wachimbaji Wadogo wa madini kupata vifaa, Serikali ilitenga kiasi cha **Shilingi bilioni 7.48** kwa ajili ya kutoa Ruzuku Awamu ya III kupitia Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini *(Sustainable Management of Mineral Resources Project – SMMRP)* unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Maombi ya Ruzuku Awamu ya III yaliyowasilishwa yamefanyiwa

*Chanzo: REA, 2017*

uchambuzi wa kina na taratibu kwa ajili ya kutolewa ruzuku hiyo zinakamilishwa. Hata hivyo, utoaji wa Ruzuku hiyo umechelewa kutokana na baadhi ya Wanufaika wa Ruzuku Awamu ya II kutumia fedha hizo kinyume na Makubaliano ya Mikataba baina yao na Serikali.

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na tatizo hilo, Wizara imewaandikia barua Wanufaika wa Ruzuku kwa kuwajulisha mapungufu ya utumiaji wa Ruzuku hiyo ili wafanye marekebisho na kwa wale watakaoshindwa warudishe fedha. Utoaji wa Ruzuku Awamu ya III utaendelea baada ya kujiridhisha na utekelezaji wa zoezi hili.

**146.** ***Mheshimiwa Spika,* natoa rai kwa Wanufaika wote wa Ruzuku kuhakikisha kuwa wanatumia fedha hizo kuendeleza Miradi ya uchimbaji na uchenjuaji madini kwa mujibu wa Mikataba yao. Wale wote watakaothibitika kutumia Fedha za Ruzuku vibaya hatua za kisheria zitaendelea kuchukuliwa dhidi yao.**

*Chanzo: REA, 2017*

**147. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini *(SMMRP)* wa Benki ya Dunia Awamu ya II inaendelea na hatua za uanzishwaji wa Vituo vya Mfano saba (7) vya kuchenjulia madini katika maeneo ya Buhemba – Mara, D-Reef na Kapanda – Mpanda, Itumbi – Chunya, Katente - Geita, Kyerwa - Kagera na Maweni Mkoani Tanga. Uanzishwaji wa Vituo hivi utagharimu Jumla ya **Dola za Marekani milioni 8.4** sawa na **Shilingi bilioni 19.41**. Vituo hivyo vitatumiwa na Wachimbaji Wadogo kuchenjua madini na kujifunza namna bora na endelevu ya kuendesha Migodi yao kitaalam na kwa tija zaidi. Kazi iliyofanyika hadi sasa ni utafiti wa kina ambapo uchorongaji wa miamba umefanyika katika maeneo hayo ili kubaini uwepo wa mashapo ya kutosha ya madini husika. Kituo cha saba (7) kitakuwa eneo la Masakasa/Mkwenyule-Wilayani Kilwa ambacho ni Kituo cha uongezaji thamani madini ya chumvi. Tayari eneo la Kituo hiki limekaguliwa na linafaa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

*Chanzo: REA, 2017*

**148. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Wizara imetoa mafunzo kwa Wachimbaji Wadogo 6,000 katika Kanda ya Kati, Kanda ya Kati Magharibi, Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Kusini, Kanda ya Kusini Magharibi, Kanda ya Mashariki, Kanda ya Ziwa Nyasa, Kanda ya Ziwa Viktoria Magharibi na Kanda ya Ziwa Viktoria Mashariki. Mafunzo hayo yalihusu masuala ya uchimbaji madini, uchenjuaji, afya na usalama Migodini, ujasiriamali na utunzaji wa mazingira na yalitekelezwa na Maafisa Madini wa Kanda na Mikoa. Zoezi hilo lilifanyika ikiwa ni sehemu ya kazi za kawaida za kupitia Bajeti za Ofisi za Kanda za Matumizi ya Kawaida.

**149. *Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Wizara itaendelea kutoa Huduma za Ugani kwa Wachimbaji Wadogo nchini. Aidha, kwa kupitia STAMICO na GST, Wizara imepanga kutoa mafunzo ya nadharia na vitendo kwa Wachimbaji Wadogo 4,000 katika Kanda za Kusini, Ziwa Nyasa, Kati na Kusini Magharibi. Pia, Wizara itaendelea kukamilisha ujenzi wa Vituo

vya Mfano na kuendelea kufanya utafiti wa kina kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya Wachimbaji Wadogo. Shughuli hizo zimetengewa Jumla ya **Dola za Marekani milioni 5.6** sawa na takriban **Shilingi bilioni 12.94** na zitagharamiwa na Mradi wa SMMRP unaofadhiliwa na Benki ya Dunia

***Uboreshaji wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini***

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuboresha huduma za utoaji na usimamizi wa Leseni za madini kwa kuwezesha malipo ya ada za Leseni za madini kufanyika kwa njia ya Mtandao *(online payments)*. Katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017, Jumla ya maombi ya Leseni 8,942 ya utafutaji na uchimbaji wa madini yalipokelewa na Wizara kwa njia ya Mtandao *(Online Mining Cadastre Transactional Portal)*. Kati ya hayo, maombi 585 ni ya utafutaji mkubwa, maombi 17 ni ya uchimbaji wa kati na maombi 8,340 ni ya uchimbaji mdogo. Baada ya uchambuzi wa maombi hayo, **Jumla ya Leseni 3,467**

*Chanzo: REA, 2017*

zilitolewa. Kati ya hizo, Leseni 296 ni za utafutaji mkubwa, 10 za uchimbaji wa kati na 3,161 za uchimbaji mdogo. Wizara itaendelea kusimamia kwa karibu utoaji wa Leseni ili kukuza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa.

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa Leseni zinazotolewa zinafanyiwa kazi, Wizara iliendelea kufuatilia Wamiliki wa Leseni na waliobainika kutotekeleza masharti husika ya Leseni hizo walifutiwa Leseni zao. Katika kutekeleza azma hiyo, **Jumla ya Leseni 2,153 zilifutwa**, kati ya hizo, Leseni 72 zilikuwa ni za utafutaji madini na 2,081 ni za uchimbaji mdogo wa madini. Aidha, hati za makosa *(default notices)* 243 zilitolewa kwa Wamiliki wa Leseni za utafutaji madini, 13 kwa Wamiliki wa Leseni za uchimbaji wa kati na 2,186 kwa Wamiliki wa Leseni za uchimbaji mdogo. **Naendelea kutoa wito kwa Wadau wa Sekta ya Madini kujisajili kwa njia ya Mtandao ili kurahisisha huduma za utoaji Leseni na kuongeza uwazi hivyo kupunguza malalamiko ya kuwepo kwa upendeleo katika utoaji wa Leseni za madini.**

*Chanzo: REA, 2017*

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara itaendelea kuboresha Mfumo wa utoaji wa Leseni na kutoa mafunzo kwa Watendaji; kuhamasisha Wadau wa madini ambao hawajasajiliwa ili waweze kutumia Mfumo huu; kufanya ukaguzi wa Leseni; na kufuta Leseni ambazo hazifanyiwi kazi.

### *Kuimarisha Usimamizi wa Migodi Nchini*

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Jumla ya Migodi 1,115 ilikaguliwa ili kuhakikisha kuwa Kanuni za Usalama, Afya na Utunzaji wa Mazingira Migodini zinazingatiwa. Kati ya Migodi hiyo, Migodi Mikubwa minne (4), Migodi ya Kati 52 na Migodi Midogo 1,059 ilikaguliwa. Ukaguzi huo umesaidia kuimarisha hali ya Afya, Usalama na Utunzaji wa Mazingira kwa Wachimbaji wa Migodi husika.

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na juhudi za Wizara katika ukaguzi wa Migodi, ajali zinaendelea kutokea hususan, kwenye

*Chanzo: REA, 2017*

Migodi ya Wachimbaji Wadogo kutokana na kutofuata Sheria na Kanuni za uchimbaji madini. Maeneo ambako ajali zimetokea kwa wingi ni maeneo yenye mifumuko ya madini *(mineral rush areas)* ambayo yanavamiwa na kuchimbwa bila leseni hususan kwenye maeneo ya hifadhi za misitu ambako Wizara ya Nishati na Madini haina uwezo wa kutoa leseni bila ridhaa ya Mamlaka husika. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Jumla ya ajali 17 zilitokea katika Migodi hiyo na kusababisha vifo vya Wachimbaji 30. Aidha, katika ajali hizo, Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Sekta ya Madini walifanikiwa kuokoa Wachimbaji 42 wakiwa hai. **Wizara inatoa shukrani za dhati kwa Viongozi wa Serikali, Kampuni za Madini, Taasisi mbalimbali, Wachimbaji Wadogo na Wadau wote walioshiriki kwa namna moja ama nyingine kuokoa maisha ya wahanga wa ajali Migodini.**

**155.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kuongezeka kwa ajali katika Migodi ya Wachimbaji Wadogo, Wizara katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 itaimarisha ukaguzi wa Migodi hiyo nchi nzima na kuwa na taarifa

*Chanzo: REA, 2017*

za kila Mwezi za Migodi yote inayofanya kazi. **Migodi yote ambayo itabainika kutokidhi vigezo vya kiusalama kwa mujibu ya Kanuni za Afya na Usalama Migodini za Mwaka 2010 itafungwa mara moja hadi marekebisho stahiki ya kiusalama yatakapofanyika na kuridhiwa na Mkaguzi wa Migodi**. Aidha, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo Wakaguzi wa Migodi kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi ili waweze kukagua Migodi kwa umakini zaidi na kupunguza matukio ya ajali.

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia utunzaji wa mazingira Migodini, Kampuni ya ACACIA inayomiliki Migodi ya Buzwagi, Bulyanhulu na North Mara imeweka Hati Fungani *(Rehabilitation Bond)* ya kiasi cha **Dola za Marekani milioni 41.10** sawa na takriban **Shilingi bilioni 94.98** kwa ajili ya kurekebisha mazingira. Mkataba wa Makubaliano hayo umepitishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kusainiwa na pande zote mbili tarehe 14 Desemba, 2016. Aidha, Hati Fungani kwa ajili ya Kampuni ya Williamson Diamonds

*Chanzo: REA 2017*

Limited inayomiliki Mgodi wa Almasi wa Mwadui inapitiwa na Wataalam wa Wizara na itawasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya ushauri wake kabla ya kusainiwa. Pia, Kampuni za Geita Gold Mining Limited, Shanta Mining Co. Limited (New Luika Gold Mine), STAMIGOLD Mine na Dangote Industries Tanzania Ltd zimewasilisha Mipango yao ya ufungaji Migodi yao kulingana na Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Kamati ya Kitaifa ya Ufungaji wa Migodi imeshaanza kupitia Mipango hiyo. Wamiliki wa Mgodi wa TanzaniteOne wameelekezwa kutayarisha Mpango wa Ufungaji Mgodi huo na kuwasilisha Wizarani mapema iwezekanavyo. Migodi ya Kati na Mikubwa yote nchini inafuata utaratibu huo kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010. Pia, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa Wachimbaji Wadogo kuhusu kuandaa Mpango wa Utunzaji Mazingira (EPP) kwa kuzingatia Sheria ya Madini ya Mwaka 2010.

**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara itakamilisha Mkataba baina yake na Kampuni ya Williamson Diamonds Limited

*Chanzo: REA, 2017*

kwa ajili ya kuweka Hati Fungani na kupitia na kukamilisha Mipango ya Ufungaji Migodi *(Mines Closure Plans)* kwa Migodi iliyobaki. Pia, Wizara kupitia *National Mine Closure Committee* itapitia na kukamilisha Mpango wa Ufungaji wa Hati Fungani kwa Migodi ya TanzaniteOne, Dangote, Geita Gold Mine, New Luika Gold Mine na STAMIGOLD.

***Usimamizi wa Masuala ya Baruti Nchini***

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Jumla ya tani 31,092 za Baruti na Vipande 3,878,607 vya Fataki viliingizwa nchini kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo uchimbaji wa madini, utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia na ujenzi wa miundombinu. Aidha, Wizara ilitoa vibali 135 vya kuingiza Baruti nchini, vibali 280 vya kulipulia Baruti na Leseni 31 za maghala ya kuhifadhia Baruti. Maghala hayo yana uwezo wa kuhifadhi Jumla ya tani 553 za Baruti *(fractured explosives)* na Vipande milioni 5.5 vya Viwashio *(detonators).*

*Chanzo: REA, 2017*

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara itaendelea kuimarisha usimamizi wa masuala ya Baruti nchini ikiwa ni pamoja na kutoa elimu na mafunzo ya matumizi bora na salama ya Baruti kwa Wachimbaji Wadogo wa madini na Wadau wengine kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali; kukagua maghala ya kuhifadhia Baruti; kusimamia matumizi sahihi ya Baruti kulingana na Sheria zilizopo sambamba na kuwasilisha Bungeni Muswada Mpya wa Sheria ya Baruti ya Mwaka 2017 kwa kuwa Sheria iliyopo ina mapungufu ya udhibiti wa matumizi mabaya ya Baruti.

***Kuhamasisha Shughuli za Uongezaji Thamani Madini***

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi 2017, Wizara ilitoa Jumla ya Leseni 40 za uchenjuaji wa marudio ya madini ya dhahabu. Aidha, ongezeko la leseni hizo limewezesha Serikali kuongeza mapato yatokanayo na shughuli za uchenjuaji dhahabu ambapo Jumla ya Mrabaha wa

*Chanzo: REA, 2017*

**Shilingi bilioni 4.23** umekusanywa. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Kituo cha Jimolojia Tanzania *(Tanzania Gemological Centre – TGC)* kilichopo Arusha kimeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi (Miezi 6) ya usanifu wa madini ya Vito *(lapidary)* ambapo wanafunzi 18 walidahiliwa Mwezi Machi, 2016 na kumaliza Septemba, 2016. Pia, wanafunzi wengine 18 walidahiliwa kuanzia Mwezi Oktoba, 2016 na wanatarajiwa kumaliza masomo yao mwishoni mwa Mwezi Mei, 2017 na hivyo kufanya Jumla ya Wahitimu wa Kituo hicho kufikia 65 tangu kuanzishwa kwa mafunzo hayo Mwezi Novemba, 2014. Mafunzo hayo yanaendelea kudhaminiwa na Mfuko wa Kuwaendeleza na Kuwajengea Uwezo Wanawake *(Arusha Gem Fair Women Foundation Fund)* ulioanzishwa kupitia Maonesho ya Vito ya Arusha.

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilianzisha taratibu za usajili wa Kituo hicho kwenye Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) katika Mwaka 2015/16. Hata hivyo, usajili wa Kituo hiki haujakamilika hadi sasa baada ya NACTE kusitisha kwa muda usajili wa vyuo nchini kwa lengo la kufanya uhakiki

*Chanzo: BEX, 2017*

wa ubora wa vyuo vilivyopo. Mara NACTE watakapoanza tena zoezi la kusajili vyuo, Wizara itahakikisha kuwa usajili wa TGC unakamilishwa haraka. Usajili ukikamilika, Kituo kinakusudia kutoa mafunzo ya Diploma ya *Gem & Jewellery Technology* ambapo mhitimu katika Mwaka wa Kwanza atapata Cheti cha *Basic Technician Certificate in Gem & Jewellery Technology (NTA Level 4)*, Mwaka wa Pili *Technician Certificate in Gem & Jewellery Technology (NTA Level 5)* na Mwaka wa Tatu *Ordinary Diploma in Gem & Jewellery Technology (NTA Level 6)*. Pia, Kituo kinatarajia kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa kozi mbalimbali za uongezaji thamani madini.

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika juhudi za kukijengea uwezo Kituo cha TGC, Wizara inawatumia Wakufunzi Waelekezi kutoka nje ya nchi na wakati huo huo inajenga uwezo wa Wakufunzi wa Kitanzania. Wizara imepeleka Watumishi watatu (3) katika nchi za Sri Lanka, India na Thailand kusomea fani za usonara *(Jewelly design & making)*, ukataji na uchongaji *(lapidary)* na jimolojia *(gemology)*. Wataalam hao wamehitimu

*Chanzo: REA, 2017*

mafunzo hayo na wameanza kazi kwenye Kituo cha TGC.

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Wizara imepanga kupeleka Watumishi wengine saba (7) kusomea fani mbalimbali za uongezaji thamani madini kupitia Mradi wa SMMRP unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Jumla ya **Shilingi milioni 694.76** zinakadiriwa kutumika kwa ajili ya kugharamia mafunzo hayo. Aidha, ili kukiongezea ufanisi, Kituo kimepewa *sub*-vote itakayoanza kutumika Mwaka wa Fedha wa 2017/18.

***Uchambuzi na Uthaminishaji wa Madini ya Vito***

**164.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Wizara kupitia TANSORT imeendelea kusimamia uthamini wa madini ya Almasi na Vito ambapo kiasi cha karati **174,700** za Almasi zenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 47.95** sawa na **Shilingi bilioni 110.81** zilithaminishwa na kusafirishwa nje ya nchi. Vilevile, Wizara

*Chanzo: REG, 2017*

ilifanya uthamini wa madini ya Vito ambapo ilithaminisha **tani 604.39** za madini ya mapambo *(Ornamental stones)*, **gramu milioni 3.30** za vito ghafi na karati **177,339** za madini ya vito yaliyosanifiwa kwa thamani ya **Dola za Marekani milioni 23.46** sawa na **Shilingi bilioni 54.22**. Kutokana na shughuli hizo, Serikali imekusanya Mrabaha wa **Dola za Marekani milioni 3.31** sawa na **Shilingi bilioni 7.65.**

**165.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Wizara itaendelea kusimamia kwa umakini zaidi shughuli ya uthaminishaji wa madini ya Almasi na Vito vingine ili kuhakikisha Serikali inapata mapato stahiki. Aidha, Wizara itaanzisha na kusimamia masoko (magulio) ya ndani ya madini ya Vito kwa kushirikiana na Ofisi za Madini za Kanda na itatoa huduma za kijimolojia kwa Wachimbaji Wadogo na wa Kati.

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** uanzishwaji wa masoko (magulio) ya ndani ya madini ya Vito unalenga kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo kwa kuwapatia soko la uhakika

*Chanzo: REA, 2017*

na bei za ushindani karibu na maeneo ya Morogoro (Mkuyuni), Merelani, Tanga na Tunduru na kupata madini yenye ubora unaohitajika katika Maonesho ya Kimataifa ya Vito ya Arusha *(Arusha Gem Fair - AGF)* ambayo hufanyika mara moja au zaidi kwa mwaka.

### *Miradi Mikubwa ya Madini*

**167.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuhamasisha na kuwezesha Kampuni za madini katika uendelezaji wa Miradi Mikubwa ya madini. Miradi hiyo ni pamoja na Miradi ya *graphite* (kinywe) iliyopo Nachu, Namangale na Chilalo Wilayani Ruangwa; Chidya na Chiwata Wilayani Masasi na Epanko, Mahenge Wilayani Ulanga. Madini ya *graphite* yanatumika kwenye kutengeneza vilainishi *(lubricants),* betri na vifaa vya kwenye injini za magari. Uwekezaji katika Miradi hiyo upo katika hatua mbalimbali za kukamilisha tathmini ya athari za mazingira na ulipaji wa fidia. Hata hivyo, Mradi wa Epanko umekumbwa na tatizo la baadhi ya Wananchi kukataa

*Chanzo: REA 2017*

kupisha maeneo yao kwa ajili ya kuanzishwa kwa Mradi huo. Wizara kwa kushirikiana na

Uongozi wa Mkoa wa Morogoro inaendelea kutoa elimu kwa Wananchi juu ya umuhimu wa Mradi huo.

**168.** ***Mheshimiwa Spika,*** Miradi mingine ambayo ipo katika hatua ya uendelezaji ni pamoja na Mradi wa Urani ambao upo eneo la Mto Mkuju katika Wilaya ya Namtumbo. Mradi huo unaendelezwa na Kampuni ya Mantra Tanzania Limited. Hata hivyo kutokana na kushuka kwa bei ya madini ya urani katika Soko la Dunia, Mradi huo umechelewa kuanza kwa kuwa uchimbaji ukifanyika sasa Serikali na Mwekezaji hawataweza kupata manufaa stahiki.

**169.** ***Mheshimiwa Spika,*** Miradi ya *Rare Earth Elements (REE)* na *niobium* iliyopo katika Wilaya ya Songwe ipo katika hatua za juu za utafiti na uanzishwaji wa Mgodi, sawia. Kukamilika na kuanzishwa kwa uchimbaji wa madini katika Miradi hii kutasaidia nchi kupata Mapato kutoka kwenye madini mengine zaidi ya dhahabu ambayo Migodi yake mingi inaendelea kufungwa kutokana na kuisha kwa mashapo katika maeneo husika.

*Chanzo: REA, 2017*

***Utatuzi wa Migogoro***

**170. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017, Wizara imeendelea na juhudi za kutatua migogoro mbalimbali katika Sekta ya Madini. Katika kipindi hicho Wizara kupitia Kamati Maalum ya Wataalam wa Serikali imefanya uhakiki kwa Wananchi wa Kitongoji cha Nyamichele Kijiji cha Nyakunguru wanaozunguka eneo la Mgodi wa Dhahabu wa North Mara ambao walifyekewa mazao yao wakati wa zoezi la kufanya tathmini ya mali na ardhi Mwaka 2013. Jumla ya Wananchi 2,742 walifanyiwa uhakiki wa maeneo yao ili kupisha shughuli za Mgodi. Lengo la uhakiki huo lilikuwa ni kubaini Wamiliki halali wa maeneo hayo ili walipwe fidia ya mazao yaliyofyekwa pamoja na gharama za usumbufu.

**171. *Mheshimiwa Spika,*** kati ya Wananchi 2,742 waliohakikiwa, Wananchi 1,586 wamebainika kutokuwa na kasoro za umiliki wa maeneo yao na Kamati ilipendekeza walipwe fidia ya mazao yao yaliyofyekwa pamoja na gharama za usumbufu. Wananchi

*Chanzo: REA 2017*

wenye umiliki wa maeneo *(parcels)* 1,016 wamebainika kuwa na kasoro mbalimbali za umiliki wa ardhi, Kamati ilipendekeza majina ya wamiliki wa maeneo hayo yachunguzwe na TAKUKURU na Vyombo vingine vya Dola ili haki itendeke.

**172. *Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kutoa muda wa kutosha kwa ajili ya uhakiki huo, Wananchi wanaomiliki maeneo (*parcels)* 139 hawakujitokeza kwa ajili ya kuhakikiwa, hivyo Kamati ilipendekeza kuwa Wananchi hao wasilipwe chochote na kama wataona hawakutendewa haki wanaweza kudai haki hiyo kupitia Vyombo vya Sheria. Aidha, pamoja na malipo hayo, Wananchi wataendelea kumiliki maeneo yao kwa kuwa Mgodi umeazimia kuendeleza uchimbaji kwa njia ya chini kwa chini *(Underground Mining).*

**173. *Mheshimiwa Spika,*** Pamoja na kushughulikia malalamiko ya fidia za Wananchi wa Kijiji cha Nyakunguru, Kamati pia ilitoa maelekezo kwa Mgodi wa North Mara kuwalipa fidia stahiki na kuwahamisha Wananchi wote walio ndani ya eneo hai la

*Chanzo: REA, 2017*

Mgodi (Mita 200) ili kupisha shughuli za Mgodi. Maeneo hayo ni yale yaliyomo katika Vijiji vya Matongo, Nyangoto, Nyabichune, Mjini Kati, Nyakunguru, Komarera na Kijiji cha Kewanja.

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imefanikiwa kutatua mgogoro wa Wananchi wa eneo la Magambazi Wilayani Handeni waliokuwa wamevamia eneo la Leseni ya uchimbaji la Kampuni ya Canaco. Wananchi hao wameondolewa katika eneo hilo na Kampuni hiyo imekubali kutoa sehemu ya eneo ndani ya Leseni kwa ajili ya kuendesha shughuli za uchimbaji kwa Wananchi hao. Aidha, Wananchi wameelekezwa kuunda vikundi na kuvisajili kabla ya kupewa Leseni za uchimbaji. Hadi sasa vikundi saba (7) vimeundwa na kusajiliwa, kikundi kimoja kimeshapewa Leseni na kimeanza shughuli za uchimbaji na vikundi vingine sita (6) viko katika utaratibu wa kupatiwa Leseni za uchimbaji mdogo. Kampuni ya Canaco imeahidi kuvipatia baadhi ya vifaa vya uchimbaji vikundi vitakavyopatiwa Leseni katika maeneo hayo.

*Chanzo: REA, 2017*

***Ushiriki wa Watanzania Katika Shughuli za Madini (Local Content)***

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuhamasisha na kutoa elimu kwa Wananchi wanaozunguka Migodi kuhusu fursa za kiuchumi zilizopo katika Migodi inayowazunguka. Kwa hali ilivyo sasa, ushiriki wa Watanzania katika kutoa huduma na kuuza bidhaa kwenye Migodi umefikia takriban **asilimia 50**. Vilevile, Wizara inaendelea kuhamasisha Migodi kutoa zabuni kwa Wananchi wanaozunguka Migodi na Kampuni za Wakandarasi wa Kitanzania ili kutoa fursa kwa Watanzania kuuza huduma na bidhaa kwenye Migodi hiyo.

**176.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuhamasisha Wamiliki wa Viwanda kutumia malighafi za madini yanayopatikana hapa nchini ili kukuza Viwanda vya Ndani. Katika kutekeleza hilo, Wizara imeweka zuio kwa Viwanda vya Saruji kuingiza malighafi (Makaa ya Mawe

*Chanzo: REA, 2017*

na Madini ya Jasi) kutoka Nje ya Nchi. Ili kuhakikisha Wamiliki wa Viwanda vya

Saruji wanapata malighafi zinazotakiwa na kwa muda muafaka, Serikali imewaelekeza kuingia Mikataba na Wachimbaji wa madini ya Jasi na Makaa ya Mawe.

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza uwazi na ushiriki wa Watanzania katika Migodi Mikubwa, Serikali kupitia Gazeti la Serikali Na. 286 la tarehe 07 Oktoba, 2016, imetunga Kanuni za Usajili wa Hisa kwa Kampuni za Madini *(The Mining (Minimum Shareholding and Public Offering) Regulations, 2016)*. Kanuni hizi zinazitaka Kampuni zenye Leseni kubwa za Uchimbaji wa Madini *(Special Mining Licence)* kuandikisha **asilimia 30** ya Hisa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam *(Dar es Salaam Stock Exchange – DSE)*. Kanuni zinazitaka Kampuni zilizopata leseni kabla ya kutangazwa kwa Kanuni kusajili **asilimia 30** ya Hisa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam ndani ya kipindi cha miaka miwili tangu kutangazwa kwa Kanuni hizi. Aidha, Kampuni ambazo zitapata leseni baada ya kutangazwa kwa Kanuni hizi zinatakiwa kutekeleza masharti ya Kanuni hizi ndani ya mwaka mmoja kutoka tarehe ya kupewa Leseni.

*Chanzo: REA , 2017*

**178.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Gazeti la Serikali Na. 44 la tarehe 24 Februari, 2017 *(The Mining (Minimum Shareholding and Public Offering) (Amendment) Regulations, 2016)*, Serikali imefanya Marekebisho ya Kanuni hizi kwa kuzitaka Kampuni ambazo zinamiliki Leseni za Uchimbaji Mkubwa zilizotolewa kabla ya kutangazwa kwa Kanuni hizi kutekeleza masharti ya Kanuni hizi ndani ya kipindi cha miezi sita (6) tangu tarehe ya kutangazwa kwa mabadiliko ya Kanuni hizo. Pia, Kampuni ambazo zitapata leseni baada ya kutangazwa kwa Kanuni hizi sasa zinatakiwa kusajili **asilimia 30** ya Hisa katika Soko la Hisa mara baada ya kuanza shughuli za uchimbaji.

**179.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa sasa kuna Jumla ya Kampuni 12 zinazomiliki Leseni 14 za uchimbaji mkubwa zinazohitajika kusajiliwa kwenye Soko la Hisa. Kampuni hizo ni Bulyanhulu Gold Mine Limited, Pangea Minerals Limited, Geita Gold Mining Limited, North Mara Gold Mine Limited (2), STAMIGOLD Company Limited, Williamson Diamonds Limited, Mantra Tanzania Limited, El-Hilal Minerals Limited,

*Chanzo: REA, 2017*

Kiwira Coal Mines Limited, Tanzania China International Mineral Resources Limited (2), Uranex Tanzania Limited na Dangote Industries Limited. Wizara imeagiza Kampuni hizo zijisajili kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam *(DSE)*.

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Wizara itaendelea kuchukua hatua za makusudi kuelimisha umma kuhusu manufaa na fursa zilizopo katika Sekta ya Madini na kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali kujenga uwezo wa Watanzania kushiriki katika Sekta hiyo. **Natoa wito kwa Wananchi kujiandaa ili Kampuni za madini zikisajiliwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam, Watanzania wajitokeze kwa wingi kununua Hisa na hivyo kushiriki kwenye umiliki wa rasilimali zao za madini.**

***Kuvutia Uwekezaji Katika Sekta ya Madini***

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Wizara imeendelea

*Chanzo: REA, 2017*

kuhamasisha na kutangaza fursa mbalimbali za uwekezaji katika Sekta ya Madini nchini kupitia Balozi za nchi mbalimbali zilizopo ndani ya nchi na Balozi zetu zilizopo nje ya nchi zikiwemo Afrika Kusini na Canada. Aidha, Wizara imefanikiwa kushiriki kwenye Mkutano Mkubwa wa kuvutia wawekezaji Afrika unaojulikana kama *Mining Indaba* – Afrika ya Kusini ambapo Serikali imetoa taarifa mbalimbali kuhusu mazingira ya uwekezaji katika Sekta ya Madini. Pia, Wizara imeshiriki katika Mikutano ya *Kimberly Process Certificate System* (KPCS) katika Nchi ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na *International Conference on Great Lakes Region* (ICGLR) katika Nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Wizara imefanikiwa kufanya Minada Miwili ya Madini ya Tanzanite Mkoani Arusha ambapo Mnada wa Kwanza ulifanyika Mwezi Agosti, 2016 na Mnada wa Pili ulifanyika Mwezi Machi, 2017. Katika Mnada wa Kwanza madini yenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 3.45** yaliuzwa

*Chanzo: REA, 2017*

na kuiwezesha Serikali kukusanya Mrabaha wa thamani ya **Dola za Marekani 150,491** sawa na **Shilingi milioni 347.78**. Katika Mnada wa Pili madini yenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 4.20** yaliuzwa na kuiwezesha Serikali kukusanya Mrabaha wa kiasi cha **Dola za Marekani 210,114.36** sawa na **Shilingi milioni 485.57**. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro ilikusanya Ushuru wa Huduma kiasi cha **Shilingi milioni 27.99**.

**183.** ***Mheshimiwa Spika,*** lengo kuu la Minada hii ni kuwakutanisha moja kwa moja Wazalishaji wa Madini ya Tanzanite, Wafanyabiashara na wenye Viwanda vya kuongeza thamani madini ili kuwezesha Wafanyabiashara kuuza madini yao kwa bei ya ushindani na Serikali kukusanya Mapato stahiki. Aidha, Minada hii husaidia kupunguza utoroshaji wa madini nje ya nchi na kuitangaza Tanzania katika medani ya Kimataifa kuhusu fursa za madini yanayopatikana nchini. Pia, Wizara ilifanya Maonesho ya Kimataifa ya Vito na Usonara, Arusha kuanzia tarehe 03 hadi 05 Mei, 2017.

*Chanzo: REA, 2017*

**184.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara itaendelea kushiriki katika Maonesho na Makongamano ya Kitaifa na Kimataifa ili kutangaza fursa za uwekezaji katika Sekta ya Madini hapa nchini. Pia, kuandaa Maonesho ya Kimataifa na Minada ya Madini ya Vito itakayohusisha Wanunuzi wa Ndani na Nje. Katika Minada ya madini ya Tanzanite Serikali itahakikisha Wauzaji wanajumuisha Tanzanite iliyokatwa ili kukuza Viwanda vya ndani vya kukata Madini ya Vito. **Natoa wito kwa Wadau wa madini ya Vito waendelee kushirikiana na Wizara ili kufanikisha Maonesho na Minada hiyo kwa lengo la kukuza Masoko ya Ndani na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini**.

***Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP) wa Benki ya Dunia***

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini *(Sustainable Management of Mineral Resource Project – SMMRP)* Awamu ya II unaofadhiliwa

*(Chanzo: REA, 2017*

na  Benki ya Dunia umeanza ujenzi wa Kituo cha mafunzo kwa Wachimbaji Wadogo cha Rwamgasa - Geita. Kituo hiki kinajengwa kwa ushirikiano baina ya Wizara, Mgodi wa Geita na Ushirika wa Wachimbaji Wadogo wa Rwamgasa. Ujenzi wa  Kituo hicho utagharimu kiasi cha **Dola za Marekani 500,000** sawa na **Shilingi bilioni 1.16** ambao unatarajiwa kukamilika ifikapo Mwezi Julai, 2017.

**186.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli nyingine za Mradi huu zilizofanyika ni pamoja na kukamilika kwa taratibu za ununuzi za kuwapata Washauri Waelekezi *(Consultants*) kwaajiliyakusanifunakusimamiaukarabatiwa Ofisi za Madini za Bariadi; Bukoba; Chunya; Kigoma; Mpanda; Musoma; Songea; Ofisi za STAMICO; na Chuo cha Madini Dodoma. Kwa sasa Mradi unaendelea na utaratibu wa kuwapata Wakandarasi ili ukarabati huo uanze. Aidha, Mradi umekamilisha ununuzi wa vifaa mbalimbali vya kutoa Huduma za Ugani kwa Wachimbaji Wadogo kupitia STAMICO, GST na Ofisi za Madini za Kanda. Shughuli hizo zimegharimu takriban **Dola za Marekani milioni 5.68** sawa na **Shilingi bilioni 13.13** na zimefadhiliwa na Benki ya Dunia.

*Chanzo: REA, 2017*

**187. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mradi wa SMMRP imewezesha GST na STAMICO kufanya utafiti wa kijiolojia katika maeneo yanayokusudiwa kuanzishwa Vituo Bora vya Mfano na maeneo mengine ya uchimbaji mdogo. Fedha zilizotumika kwa ajili ya kazi hii ni **Dola za Marekani milioni 3.7** sawa na **Shilingi bilioni 8.55** ambazo zimetolewa na Benki ya Dunia. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 kupitia Mradi wa SMMRP, Wizara inatarajia kuanza ukarabati na upanuzi wa Ofisi za Madini za Bariadi; Bukoba; Chunya; Kigoma; Mpanda; Musoma; Songea; Ofisi za STAMICO; na Chuo cha Madini Dodoma. Lengo la ukarabati ni kuboresha mazingira ya kazi ya Ofisi hizo ikiwa ni pamoja na kuongeza vyumba vya mikutano na madarasa vitakavyotumika kufundishia Wachimbaji Wadogo (*Centres of Excellence*). Vilevile, Wizara itaanza ujenzi wa Vituo vya Mafunzo (*Demonstrating Centres)* vitatu (3) katika Awamu ya Kwanza kwenye maeneo ya Itumbi (Chunya), Katente (Bukombe) na Mkwanyule (Kilwa).

*Chanzo: REA, 2017*

***Wakala wa Jiolojia Tanzania (Geological Survey of Tanzania - GST)***

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017, Serikali kupitia Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST) iliendelea kukusanya taarifa za Jiosayansi na kuchora Ramani kwa ajili ya kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Madini. GST kwa kushirikiana na *Geological Survey of China* wamefanya na kukamilisha utafiti wa Jiokemia katika Mikoa ya Mbeya na Songwe ambao ulifadhiliwa na Serikali ya China. Pia, GST kwa kushirikiana na *Geological Survey of Finland* na Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA) imetengeneza Ramani za Jiokemia za nchi nzima *(Country Wide Multi-Element Geochemical Maps)* zinazoainisha wingi wa madini ya aina mbalimbali za metali (kama dhahabu, shaba, chuma, nikeli, bati n.k.) katika sehemu mbalimbali za nchi. Mradi huu umefadhiliwa na Serikali ya Finland kwa kiasi cha **Euro 750,000** sawa na takriban **Shilingi bilioni 1.59**.

*Chanzo: REA, 2017*

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala unaendelea na kazi ya utafiti wa uchenjuaji ili kuongeza thamani ya madini ya Nikeli kwa Wachimbaji Wadogo wa Milima ya Mwahanza Haneti Dodoma. Wakala umekamilisha utafiti wa uchenjuaji wa madini ya Shaba katika Wilaya za Mpwapwa na Kilosa kwa lengo la kuongeza thamani ya madini ya Shaba. Pia, Wakala uliendelea kutoa Huduma za Maabara za uchunguzi na upimaji wa sampuli za Jiotekinolojia kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu kwa Wateja mbalimbali wakiwemo Chuo Kikuu cha Dodoma na Mgodi wa Almasi wa Mwadui.

**190.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walifanya utafiti wa Tetemeko la Ardhi lililotokea Mkoani Kagera tarehe 10/9/2016 na kuandaa taarifa za utafiti. Pia, Wataalam kutoka Wakala, Chuo Kikuu cha Ardhi na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walitoa elimu kwa umma na kwa wahanga wa Tetemeko hilo. Aidha, Wakala uliendelea kukusanya takwimu kutoka Vituo nane (8) vya kudumu vilivyoko nchini vya kupimia Matetemeko ya Ardhi, kuchakata takwimu, kuchora Ramani

*Chanzo: REA, 2017*

na kuzihifadhi kwenye kanzidata *(database)* kisha kuzitolea taarifa.

**191. *Mheshimiwa Spika,*** Wakala kwa kushirikiana na *Geological Survey of Finland* (GTK), umechapisha Ramani za Jiolojia za *block* ya Nachingwea-Masasi/Tunduru na taarifa *(Explanatory Notes)* zake baada ya kupata matokeo kutoka Maabara za GST, SUA pamoja na GTK-Finland. Vilevile, Wakala umekusanya takwimu katika maeneo ya Wilaya za Kondoa na Singida unaolenga kupata vyanzo vya nishati ya Jotoardhi kwa ajili ya uzalishaji umeme na umefadhiliwa na USAID kwa thamani ya **Shilingi milioni 33.44.** Utafiti huu unafanyika chini ya Mradi wa "*Partnership for Enhanced Engagement in Research Project (PEERP)*", unaofadhiliwa na Serikali ya Marekani.

**192. *Mheshimiwa Spika,*** Wakala umeanzisha Mfumo wa kuuza na kusambaza Ramani mbalimbali za Jiolojia na Jiofizikia, taarifa na takwimu kwa Wadau mbalimbali kwa njia ya Mtandao *(data sales portal)* na inaendelea kuimarisha na kuboresha Mfumo wa kuchakata, kutunza na kusambaza

*Chanzo: REA, 2017*

takwimu na taarifa za Jiosayansi kwa Wadau *(Geological and Mineral Information System – GMIS).*

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Wakala umepanga kuendeleza tafiti na kukusanya taarifa za Jiosayansi kwa ajili ya kuchora Ramani nne (4) za Jiolojia za Mfumo wa QDS kwa skeli ya 1:100,000 (QDSs 264, 275, 276 na 277) na Ramani nyingine mbili za Jiokemia za Mfumo wa QDS (QDS 264 na 275) kwenye maeneo yaliyopo katika Wilaya za Songea Vijijini, Ludewa na Madaba. Pia, Wakala umejipanga kufanya uhakiki maalum *(field checks)* wa Jiolojia, Jiokemia na kuboresha Ramani za QDS 49, 64 na 65 na kukusanya na kuhakiki taarifa za uwepo wa madini nchini na kuboresha kanzidata yake.

**194.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala utaendelea kuratibu majanga asilia ya Kijiolojia ikiwa ni pamoja na Matetemeko ya Ardhi, Milipuko ya Volkano, Maporomoko ya Ardhi (uchunguzi wa Jiomofolojia) ili kubaini maeneo yenye hatari ya kupata Maporomoko

*Chanzo: REA, 2017*

ya Ardhi na kutoa ushauri kwa Wananchi waishio katika maeneo hayo. Aidha, Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa Wakala kwa kununua vifaa vya utafiti wa Kijiolojia na Maabara. Wakala wa Jiolojia ulichakata takwimu na taarifa mbalimbali za Matetemeko ya Ardhi zilizokusanywa kuanzia Mwaka 1900 kuhusu mahali yalipowahi kutokea pamoja na ukubwa wake katika Mji wa Dodoma. Hii itawezesha kuainisha maeneo yenye Mipasuko chini ya Ardhi ambayo yana uwezekano mkubwa wa kutokea Matetemeko. **Ramani zinazoonesha taarifa hizi zinaweza kutumika katika upangaji bora wa Mji wa Dodoma, hivyo nachukua fursa hii kuwashauri Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma na Wadau wengine kushirikiana na GST katika kupanga matumizi bora ya Ardhi.**

### *Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA)*

**195.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2009 Serikali ilianzisha Wakala maalum kwa ajili ya Ukaguzi wa Shughuli za Uwekezaji katika

*Chanzo: REA, 2017*

Sekta ya Madini (TMAA). Kazi kubwa ikiwa ni pamoja na kukagua gharama za uwekezaji wa makampuni makubwa, mapato yatokanayo na uwekezaji huo, kodi pamoja na mrabaha unaolipwa Serikalini. TMAA hufanya kazi kwa kushirikiana na Ofisi za Madini za Kanda husika, TRA, pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani. Utendaji wa Taasisi hiyo uliendelea kuonesha mapungufu katika Sekta kwa kubaini mianya ya upotezaji wa mapato ya Serikali. Pamoja na utendaji huo, wadau mbalimbali wakiwemo Wananchi wa kawaida waliendelea kupaza sauti wakidai Taifa linaibiwa kupitia miradi ya madini.

**196.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia maoni na ushauri wa wadau, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kulinda maslahi ya Taifa. Serikali imeandaa na kuwaongezea uwezo watendaji, imepanga watendaji wenye ujuzi katika maeneo ya migodini, mipakani, viwanja vya ndege na kwenye bandari zilizopo nchini. Kutokana na jitihada hizo, kwa Mwaka 2016/17, Wakala uliweza kukamata madini yenye jumla ya thamani ya **Dola za Marekani 119,906.45** sawa na **Shilingi milioni 277.10** katika

*Chanzo REA, 2017*

viwanja vya ndege vya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza na Songwe.

**197.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Wakala ulifanya ukaguzi na kuwezesha Serikali kukusanya mrabaha wenye thamani ya **Shilingi bilioni 4.45** ikilinganishwa na jumla ya **Shilingi bilioni 6.27** zilizokusanywa kwa kipindi cha Mwaka 2015/16. Kupatikana kwa kiwango kidogo cha mrabaha, kushuka kwa mrabaha uliokusanywa kwa Mwaka 2016/17 na vilio vya wananchi kulipelekea Serikali kuchua hatua mbalimbali ili kuhakikisha Serikali inapata mapato stahiki na kukuza Pato la Taifa.

**198.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa Mwaka wa Fedha 2017/18, Serikali itaimarisha Wakala wa Ukaguzi wa Madini (TMAA) kwa kuzingatia maoni na ushauri wa wadau mbalimbali. Ushauri uliotolewa na Kamati Maalum za Bunge pamoja na Kamati Maalum ya Wataalam iliyoundwa rasmi na Mheshimiwa Rais kuchunguza mchanga uliomo katika makontena ya makinikia ya dhahabu utazingatiwa. Lengo la jitihada hizi

*Chanzo: REA, 2017*

ni kuhakikisha kwamba Taifa linanufaika kikamilifu kutokana na rasilimali za madini.

***Shirika la Madini la Taifa (State Mining Corporation – STAMICO)***

**199.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017, STAMICO kupitia Kampuni yake Tanzu ya STAMIGOLD imezalisha Jumla ya wakia 12,092 za Dhahabu na wakia 1,659 za madini ya Fedha *(silver)* na kuiingizia Kampuni **Shilingi bilioni 36.88**. Kampuni pia ililipa Serikalini Mrabaha wa **Shilingi bilioni 1.48**.

**200.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia uchimbaji unaofanyika kwa ubia kati ya STAMICO na Kampuni ya TanzaniteOne Mining Limited (TML), Jumla ya kilo 2,872.79 za Tanzanite zilizalishwa na kuuzwa kwa kipindi cha Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 ambapo Jumla ya **Shilingi bilioni 16.93** zilipatikana na **Shilingi milioni 846.5** zililipwa Serikalini kama Mrabaha.
*Chanzo: REA, 2017*

**201.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na hatua hizo, STAMICO pia inaendelea kutekeleza Mradi wa ununuzi wa madini ya Bati kutoka kwa Wachimbaji Wadogo walioko Kyerwa Mkoani Kagera ambapo hadi kufikia Machi, 2017 tani 18.08 za madini hayo ziliuzwa na kulipatia Shirika Jumla ya **Shilingi milioni 325.49** ambazo zimewezesha ulipaji wa Mrabaha kwa Serikali wa kiasi cha **Shilingi milioni 13.02** na **Shilingi 976,471** zimelipwa kama ushuru wa Huduma kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa. Aidha, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Januari hadi Machi, 2017 Jumla ya kilo 1,205 za madini ghafi ya Bati zimenunuliwa kwa Jumla ya **Shilingi milioni 22.90**.

**202.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukidhi mahitaji ya Makaa ya Mawe nchini, STAMICO imeanza rasmi uchimbaji wa Makaa hayo katika Kilima cha Kabulo - Kiwira kuanzia Mwezi Aprili, 2017 ambapo Jumla ya tani 107,078 zinakadiriwa kuchimbwa kwa Mwaka na Mradi huu utagharimu kiasi cha **Shilingi bilioni 2.39**. Lengo la Mradi huu ni kuwauzia Makaa ya Mawe Viwanda vya Saruji na watumiaji wengine.

*Chanzo: REA, 2017*

**203. *Mheshimiwa Spika,*** Shirika limefanikiwa kufanya kazi ya ukadiriaji na uthaminishaji wa mashapo ya madini yaliyopo kwenye Mradi wake wa dhahabu wa Buhemba ambapo kiasi cha wakia 441,772 za dhahabu *(indicated resources)* zimekadiriwa kuwepo katika mashapo hayo. Aidha, Mwezi Juni, 2017 kazi za ukadiriaji na uthamini wa mashapo zitafanyika katika mashimo ya Buhemba *Main* na Mwizi na kazi hizo zitakapokamilika zitawezesha ongezeko la mashapo yanayokadiriwa kufikia wakia 600,000. Mpango uliopo ni kutafuta Mwekezaji wa kuingia naye Ubia.

**204. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Shirika limeendelea kufanya tathmini za uwepo wa mashapo katika Leseni zake za madini inazozimiliki. Leseni zilizofanyiwa utafiti ni Leseni ya dhahabu iliyopo Busanda – Mkoani Geita na Madini ya *Rare Earth Elements - REE* iliyopo Sengeri Mkoani Songwe. Pia, Shirika limepata Leseni 20 za uchimbaji madini mdogo (PML) wa kokoto katika maeneo ya Chigongwe Dodoma

*Chanzo: REA, 2017*

na Ubena Zomozi Pwani ambazo zitawezesha uanzishaji wa Mradi wa kokoto katika maeneo

hayo. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 jumla ya **Shilingi bilioni 2.64** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza Mradi huu.

**205.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017, STAMICO imeendelea kutoa huduma za kitaalam kwa Wachimbaji Wadogo nchini. Jumla ya Wachimbaji Wadogo 15 wamefanyiwa utafiti wa Kijiolojia katika maeneo ya Lwamgasa - Geita (Blue Reef), Bukandwe - Mbogwe, Nyampalahala – Bukombe (Paso Mine), Mpinga-Bahi, Mkalama na Mandawa-Rwanga (Mkalama Copper Gold Project), Kazikazi – Itigi, Kiteto, Wami - Pangani (Jiwe Project), Kerezia na Ng'anzo – Bukombe, Nsagali Gold Mine na Makangaga – Kilanjelanje - Kilwa *(Mishangu International)*. Tafiti hizo zimewezesha Wachimbaji hao kupata taarifa za uwepo wa madini katika maeneo yao ambazo wanaweza kuzitumia kupata mikopo kutoka Taasisi za Fedha. Wachimbaji waliofaidika na taarifa hizo za utafiti na waliofanikiwa kupata mikopo kutoka Benki ya Uwekezaji Nchini - TIB ni Nsagali Gold Mine na Makangaga-Kilanjelanje - Kilwa (*Mishangu International*).

*Chanzo: REA, 2017*

**206. *Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017 STAMICO kwa kushirikiana na GST chini ya Mradi wa SMMRP unaofadhiliwa na Benki ya Dunia imefanya utafiti wa Kijiosayansi unaohusisha uchorongaji wa miamba na ukadiriaji wa mashapo ya madini katika maeneo yanayotarajiwa kuanzisha Vituo vya Mfano vya uchenjuaji wa madini kwa Wachimbaji Wadogo katika maeneo ya Itumbi (Chunya), Katente (Bukombe) na Kapanda (Mpanda). Katika kipindi hiki Jumla ya mita 4,138 za *Reverse Circulation (RC)* na mita 5,201 za *Diamond Drilling (DD)* zilichorongwa kwenye maeneo hayo. Aidha, STAMICO itaendelea kuboresha taarifa zinazohusu Wachimbaji Wadogo pamoja na upatikanaji wa masoko ya madini nchini kupitia Tovuti ya Wachimbaji Wadogo ya STAMICO *(Small Scale Mining Portal – www. ssm-stamico.co.tz)* na Mfumo wa utoaji wa taarifa hizo kupitia simu za kiganjani.

**207. *Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Shirika litaendelea kufanya tafiti katika maeneo yake ya Busanda (Dhahabu), Sengeri *Southern Extension (Rare Earth Elements)* na Mingoyo

*Chanzo: REA, 2017*

Lindi *(Graphite)* pamoja na kutoa Huduma za kibiashara za ushauri wa kitaalam *(Consultancy)* katika Sekta ya Madini.

**208.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Shirika pia limepanga kuendelea kuchimba Makaa ya Mawe katika Leseni yake ya Kilima cha Kabulo – Kiwira ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 10** kimetengwa na Serikali kwa ajili ya kuendeleza Mradi huo. Aidha, Shirika linaendelea kukamilisha ukadiriaji wa mashapo ya dhahabu pamoja na usanifu wa Mgodi katika Mradi wa Buhemba pamoja na kutafuta Mbia mwenye uwezo ili kuendeleza Mradi huo. Pia, Shirika litaendelea kusimamia Miradi yake ya STAMIGOLD pamoja na Miradi ya Ubia ikiwemo TanzaniteOne ili kuongeza ufanisi na Mapato ya Serikali.

*Chanzo: REA, 2017*

***Asasi ya Uwazi Katika Rasilimali za Madini na Gesi Asilia (Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative – TEITI)***

**209.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai 2016 hadi Machi, 2017 TEITI imeandaa Mpango-Kazi *(Road Map)* wa kuanzisha Rejista ya Majina na taarifa za Watu Wanaomiliki Hisa katika Leseni na Mikataba ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia kama ilivyoahidiwa na Mhe. Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) alipomwakilisha Mheshimiwa Rais katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi kuhusu Kudhibiti Rushwa *(London, Anti-corruption Summit, 2016)* uliofanyika Nchini Uingereza, tarehe 12 Mei, 2016. Aidha, TEITI imefanya mapitio ya Sheria *(Legal Review Study)* kwa ajili ya maandalizi ya uanzishaji wa Rejista hiyo. Lengo ni kubaini kama kuna vipengele katika Sheria zilizopo vinavyokataza uwekaji wazi wa majina ya watu wanaomiliki hisa katika Leseni na Mikataba ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia, hasa Sheria ya Kampuni ya Mwaka 2002 *(Companies Act, 2002)* kwa ajili ya kuvifanyia marekebisho.

**210.** ***Mheshimiwa Spika,*** maandalizi kwa ajili ya ukusanyaji wa Takwimu za Kodi zilizolipwa na Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia katika Mwaka wa Fedha wa 2014/15 na 2015/16 yamekamilika. Maandalizi hayo yamezingatia maelekezo ya Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini yaliyotolewa Mwezi Oktoba, 2016 kwa kukusanya na kuweka wazi takwimu za misamaha ya kodi, matumizi ya mafuta na mishahara ya Wafanyakazi wa Kigeni. Ripoti zitatolewa kwa umma kuanzia Mwezi Juni, 2017.

**211.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza matakwa ya Sheria ya TEITI ya Mwaka 2015 Kifungu 16 (1)(a) kinachomtaka Waziri kuweka wazi Mikataba ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia, Mwezi Desemba, 2016 Wizara ilizitaarifu Kampuni zenye Mikataba ya Madini na Gesi Asilia (MDAs na PSAs) kwamba inakusudia kuweka wazi Mikataba hiyo. Kampuni hizo zinatakiwa kuifahamisha TEITI kwa mujibu wa Kifungu 27 (2) kama kuna sehemu ndani ya Mikataba hiyo ambayo kibiashara ni muhimu kutowekwa wazi. Kati

*Chanzo: REA, 2017*

ya Kampuni 24, Kampuni nne (4) za madini na 20 za Mafuta na Gesi Asilia, Kampuni mbili (2) zimewasilisha maombi TEITI ambayo hivi sasa yanafanyiwa kazi. Aidha, maandalizi yanafanyika ili kuweka wazi Mikataba ya Kampuni hizo kwenye Tovuti za Wizara.

**212.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 TEITI itakamilisha na kutoa kwa Umma Ripoti ya Malipo ya Kodi yanayofanywa na Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia kwa Serikali kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2016/17. Aidha, TEITI itaendelea kuelimisha Umma juu ya matumizi ya takwimu zinazotolewa katika Ripoti zake ili waweze kutumia takwimu hizo katika kuhoji uwajibikaji wa Serikali.

***Chuo cha Madini Dodoma (Mineral Resources Institute – MRI)***

**213.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2016 hadi Machi, 2017, Chuo kimedahili Jumla ya **wanafunzi 527** katika fani za Jiolojia na Utafutaji Madini; Uhandisi Migodi; Uhandisi Uchenjuaji Madini; Sayansi za Mafuta na

*Chanzo: REM, 2017*

Gesi Asilia; na Uhandisi na Usimamizi wa Mazingira Migodini. Pia, Chuo kimeandaa Mtaala mpya wa Upimaji Ardhi na Migodi *(Curriculum for Land and Mine Surveying)* ambao umewasilishwa NACTE kwa ajili ya usajili. Aidha, Chuo kimefanya upanuzi na ukarabati wa Ofisi na madarasa, ujenzi wa ukumbi wa mihadhara pamoja na viwanja vya michezo kupitia Mradi wa SMMRP unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Pia, Wizara imetoa Jumla ya **Shilingi milioni 148.03** kwa ajili ya ufadhili kwa **vijana 71** wanaosoma fani mbalimbali za madini, Mafuta na Gesi Asilia katika Chuo hiki.

**214.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Chuo kitaendelea kupanua wigo wake wa kutoa mafunzo kwa kuanzisha programu mpya ya Upimaji Ardhi na Migodi. Pia, Chuo kimekusudia kuandaa Mtaala wa Wachimbaji Wadogo kwa ajili ya Watendaji wa kada ya kati watakaoweza kujiajiri kama Wachimbaji Wadogo wenye ujuzi au kufanya kazi moja kwa moja na Wachimbaji Wadogo wengine kote nchini. Aidha, Chuo kitaendelea kuwajengea uwezo Watumishi wake na pia kuendelea kuimarisha miundombinu yake muhimu.

*Chanzo: REA, 2017*

## C. AJIRA NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU

**215.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili Watumishi wa Wizara waweze kufanya kazi kwa weledi na ufanisi zaidi ikilenga kuinua mchango wa Sekta za Nishati na Madini kwenye Pato la Taifa, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Wizara iliandaa Mpango wake wa mafunzo kwa kipindi husika. Kupitia Mpango huo, Wizara ilipanga kupeleka Watumishi 87 katika mafunzo ya muda mrefu na Watumishi 166 katika mafunzo ya muda mfupi. Mpango huo unaendelea kutekelezwa ambapo hadi kufikia mwishoni mwa Mwezi Machi, 2017, Watumishi 67 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi. Kati ya hao 2 wanasomea Shahada ya Uzamivu, 43 Shahada ya Uzamili, 16 shahada ya kwanza na 6 Stashahada. Aidha, katika kipindi hicho Wizara ilipeleka Watumishi 28 katika mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi. Mafunzo hayo yalitolewa katika fani mbalimbali zikiwemo: Uthaminishaji, Ukataji na Utafiti wa Vito; Uhandisi Migodi; Jiolojia; Fedha; Uhasibu na Usimamizi katika masuala ya Mafuta na Gesi Asilia; Usimamizi

*Chanzo: REA 2017*

wa Mazingira; Uchumi na Sera za Umma; Sheria hususan katika Mafuta na Gesi Asilia; Petroli; na masuala ya Jiosayansi kwa ujumla. Pamoja na mafunzo haya kufanyika nchini, Watumishi walihudhuria mafunzo nje ya nchi zikiwemo: Australia, Brazil, China, India, Norway, Sri Lanka, Thailand na Uingereza. Mafunzo hayo ya muda mrefu na muda mfupi kwa ujumla yaligharimu Jumla ya **Shilingi bilioni 1.41** zikiwa ni fedha za Ndani na Nje zilizotengwa na Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17.

**216.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafunzo hayo, Wizara pia iliendelea kushirikiana kwa karibu na Washirika wa Maendeleo ili kupata ufadhili wa masomo kwa Watanzania wanaokidhi vigezo katika nchi mbalimbali kwenye mafunzo ya Shahada za Uzamili na Uzamivu. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Watanzania 16 walipata ufadhili wa kusomeshwa nchini China Shahada ya Uzamili na wawili (2) Shahada ya Uzamivu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China katika masuala ya Mafuta na Gesi Asilia.

*Chanzo: REA, 2017*

**217.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kuwapa Watumishi ujuzi mbalimbali kwa ajili ya kuinua utendaji wao, Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 imepanga kuwapeleka Jumla ya Watumishi 227 katika mafunzo ya fani mbalimbali zikiwemo: Usimamizi wa Rasilimali za Mafuta na Gesi Asilia; Sheria; Uchumi; Jiolojia; Jemolojia; pamoja na Fedha na Uhasibu katika masuala ya Mafuta na Gesi Asilia. Kati ya Watumishi hao, 77 watahudhuria mafunzo ya muda mrefu na Watumishi 150 mafunzo ya muda mfupi. Katika kipindi hiki Wizara imetenga Jumla ya **Shilingi milioni 679.73** kwa ajili ya kuwezesha mafunzo hayo.

**218.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha ustawi na afya za Watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI waliojitokeza, Wizara imeendelea kuwawezesha Watumishi 10 kwa kuwapa huduma ya lishe na dawa kwa kuzingatia Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 2 wa Mwaka 2006. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara itaendelea kutoa elimu mahali pa kazi ili kuzuia maambukizi mapya na kuwahudumia waathirika wa UKIMWI kadri watakavyojitokeza na Jumla

*Chanzo: REA, 2017*

ya **Shilingi milioni 12** zimetengwa kwa ajili hiyo. Sambamba na jitihada hizo, Wizara pia itaendelea kuhamasisha Watumishi kupima afya zao mara kwa mara ili kujua kama wana Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) kama vile magonjwa ya shinikizo la damu, kisukari na saratani ili waweze kuchukua hatua stahiki mapema. Aidha, Wizara itaendelea kuwahamasisha Watumishi juu ya umuhimu wa kufanya mazoezi ili kuimarisha afya zao kwa ajili ya kuendelea kulitumikia Taifa letu ipasavyo na kwa ufanisi zaidi.

**219. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuwapa motisha na kuongeza tija kwenye utendaji kazi kwa Watumishi wake, Wizara imeendelea kubuni njia mbalimbali ikiwemo ya kuwapandisha vyeo Watumishi wake. Katika kutekeleza dhana hii, kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 Wizara inatarajia kuwapandisha vyeo Jumla ya Watumishi 360 ambao wamepata sifa za kitaaluma na wenye utendaji mzuri wa kazi kulingana na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 1999.

*Chanzo: REA, 2017*

## D. WIZARA YA NISHATI NA MADINI KUHAMIA DODOMA

**220. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Nishati na Madini inaunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Tano iliyoamua kwa dhati kutekeleza maamuzi ya Mwasisi wa Taifa letu, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ya Mwaka 1973 ya kuufanya Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi yetu ambapo pia maamuzi hayo yamesisitizwa kwenye Ilani ya CCM ya Mwaka 2015 – 2020 katika Ibara ya 151 kuhusu kuhamishia Makao Makuu Dodoma. Katika kutekeleza Maamuzi hayo, Wizara imeanza kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa zoezi hilo ambalo linatekelezwa kwa awamu. Katika Awamu ya kwanza, tarehe 10 Februari, 2017 Wizara ilihamisha Watumishi 47. Awamu hii ilihusisha Watumishi wa ngazi mbalimbali wakiwemo Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu, Makamishna, Wakurugenzi na Maafisa. Kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara itaendelea kutekeleza Maamuzi hayo ambapo katika kipindi hicho Watumishi 107 wanatarajiwa kuhamishwa kuanzia Mwezi Agosti, 2017.

*Chanzo: REA, 2017*

## E. UIMARISHAJI WA MAWASILIANO KATI YA WIZARA NA JAMII

**221.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na Mpango wake wa utoaji taarifa mbalimbali kuhusu utekelezaji wa shughuli zake kupitia Kitengo chake cha Mawasiliano Serikalini. Katika Mpango huo, Wizara imeandaa na kuchapisha Matoleo ya Majarida 40 kuhusu habari za kila Wiki za Wizara na Taasisi zake. Majarida yamesambazwa kwa Wananchi, Balozi za Tanzania nje ya nchi, mitandao ya kijamii, makundi ya *WhatsApp*, Tovuti ya Wizara, vyombo vya habari na Maafisa Habari wa Taasisi mbalimbali. Kupitia Mpango huu zaidi ya wadau 7,500 wamepata taarifa hizo. Katika kipindi hiki pia, Wizara iliwahabarisha Wananchi na Wadau mbalimbali kuhusu masuala yanayoendelea katika Sekta za Nishati na Madini kupitia vyombo mbalimbali vya habari vikiwemo radio, magazeti, tovuti na televisheni.

**222.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia imeendelea kutoa elimu kwa Wananchi katika maeneo mbalimbali kwa kutumia gari lake la matangazo ambalo kimsingi

*Chanzo: REA, 2017*

limekuwa chachu ya kuzitangaza shughuli muhimu zinazotekelezwa na Wizara katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu yakiwemo ya uchimbaji mdogo wa madini. Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Wizara itaendeleza juhudi hizo kwa kutoa elimu kwa Wananchi wengi zaidi.

## F. USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

**223.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutambua michango ya Washirika wa Maendeleo ambao wamekuwa mstari wa mbele kuunga mkono juhudi za Serikali za kuleta maendeleo kwa kupitia misaada yao mbalimbali kwenye Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Sekta za Nishati na Madini. Kwa niaba ya Serikali, napenda kutoa shukrani za dhati kwa: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Maendeleo ya Afrika Kusini (DBSA), Benki ya Dunia (WB), Benki ya Exim ya China, Benki ya Ushirikiano wa Kimataifa ya Japan (JBIC), Benki ya Maendeleo ya Kiarabu *(BADEA),* Benki ya Unicredit Austria, *Climate Investment Fund* (CIF), *Economic Development Cooperation Fund* (EDCF), *OPEC Fund for International*

*Chanzo: REA, 2017*

*Development* (OFID), Mfuko wa Uendelezaji Jotoardhi (GRMF) pamoja na Taasisi na Mashirika ya: AFD (France), Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP), ICEIDA (Iceland), CIDA (Canada), DfID (UK), IDA (Benki ya Dunia), JICA (Japan), KfW (Germany), GIZ (Germany), NORAD (Norway), NDF (Nchi za Nordic), Sida (Sweden), Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), *The Nertherlands* (DRIVE) na USAID (United States of America); na nchi za Brazil, Denmark, Finland, Germany, Iceland, Norway na Korea ya Kusini. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini itaendeleza ushirikiano na Washirika hawa na wengine wa Maendeleo ili kuendeleza miradi mbalimbali.

## G. SHUKRANI

**224.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nimalizie kwa kumshukuru kwa dhati Mhe. Dkt. Medard Matogolo Chananja Kalemani, Mbunge wa Chato, Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa ushirikiano anaonipatia katika kusimamia Sekta za Nishati na Madini. Nakiri

wazi kuwa michango yake imekuwa msaada mkubwa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku ya Wizara na kitaifa kwa ujumla.

**225.** ***Mheshimiwa Spika,*** ni wazi kuwa mafanikio yote ya Wizara yanategemea ushirikiano wa Watendaji Wakuu na Wataalam mbalimbali. Hivyo, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru Naibu Makatibu Wakuu Prof. James Epiphan Mdoe pamoja na Dkt. Mhandisi Juliana Leonard Pallangyo, Makamishna, Wakurugenzi, Wakuu wa Idara na Vitengo pamoja na Watumishi wote wa Wizara. Watendaji hao wa Wizara wamekuwa makini katika kunipa ushauri na ufafanuzi katika maeneo mbalimbali ya kiutendaji, hali ambayo imenisaidia katika kuiongoza Wizara kwa ufanisi na hatimaye kuleta mafanikio makubwa.

**226.** ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue pia fursa ya kipekee kuwashukuru Wakuu wote wa Taasisi, Wenyeviti wa Bodi na Wajumbe wa Bodi za Taasisi pamoja na

*Chanzo: REA, 2017*

Watumishi mbalimbali wa Taasisi zilizo

chini ya Wizara yetu kwa ushirikiano wao wanaonipatia katika kutekeleza majukumu tuliyopewa. Ni matumaini yangu kuwa ushirikiano huu utazidi kuendelezwa siku zijazo kwa lengo la kuinua mchango wa Sekta za Nishati na Madini katika Pato la Taifa.

**227.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee napenda kumshukuru tena Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyojitoa kusimamia rasilimali za nchi hii kwa maslahi mapana ya wananchi na Taifa letu. Ninawashukuru wananchi wanaojitokeza kumuunga mkono Mheshiwa Rais na kumuombea kila anapochukua hatua ili kuwaletea maendeleo Watanzania. Hakika kiongozi wetu mkuu anastahili maombi.

*Chanzo: REA, 2017*

## H. HITIMISHO

**228.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 pamoja na kutumika katika kutekeleza shughuli mbalimbali, imelenga katika kutekeleza Miradi Mikubwa ya Nishati ili kuchochea Sekta nyingine za kiuchumi na hivyo kukuza uchumi wa Taifa letu na maendeleo ya Watanzania kwa ujumla. Wizara pia katika kipindi hiki itaendelea kwa kasi na utekelezaji wa maelekezo ya Serikali ya Awamu ya Tano ya upatikanaji wa Nishati ya uhakika ili kuwezesha kufikiwa kwa lengo la Tanzania kuwa Nchi ya Viwanda. Katika kutekeleza azma hiyo, sehemu kubwa ya Fedha za Miradi ya Maendeleo ambazo ni **Shilingi bilioni 756.76**, sawa na **asilimia 80.6** ya Fedha zote za Maendeleo zimeelekezwa katika kutekeleza Miradi ya kimkakati ya Nishati.

**229.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Jumla ya **Shilingi 998,337,759,500** kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18. Mchanganuo wa Bajeti hiyo ni kama ifuatavyo:

*Chanzo: REA, 2017*

(i) **Shilingi 938,632,006,000**, sawa na **asilimia 94** ya Bajeti yote ya Wizara ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 763,304,679,000**, sawa na **asilimia 81** ya fedha zote za Maendeleo ni Fedha za Ndani na **Shilingi 175,327,327,000**, sawa na **asilimia 19** ni Fedha za Nje.

(ii) **Shilingi 59,705,753,500**, sawa na **asilimia 6** ya Bajeti yote ya Wizara ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 28,833,681,500,** sawa na **asilimia 48.3** ya fedha zote za Matumizi ya Kawaida ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo *(Other Charges – O.C.)* na **Shilingi 30,872,072,000**, sawa na **asilimia 51.7** zitatumika kulipa Mishahara ya Watumishi *(Personnel Emolument – P.E)* wa Wizara na Taasisi zake.

*Chanzo: REA, 2017*

**230.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani ya www. mem.go.tz. Vilevile, Hotuba hii ina vielelezo mbalimbali kwa ajili ya ufafanuzi wa masuala muhimu yanayohusu Sekta za Nishati na Madini.


**231.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

*Chanzo: REA, 2017*

## VIELELEZO VYA HOTUBA YA MWAKA WA FEDHA WA 2017/18 KUHUSU SEKTA ZA NISHATI NA MADINI

### A: SEKTA YA NISHATI


***Kielelezo Na. 1:*** *Mgawanyo wa Ufuaji Umeme katika Gridi ya Taifa*




*Chanzo: TANESCO, 2017*

*Chanzo: REA, 2017*


***Kielelezo Na. 2:*** *Mauzo ya Umeme kwa Wateja Mbalimbali*




*Chanzo: TANESCO, 2017*

*Chanzo: REA, 2017*


***Kielelezo Na. 3:*** *The National Grid System*




*Chanzo: TANESCO, 2017*


*Chanzo: REA, 2017*

***Kielelezo Na. 4:*** *Percentage Distribution of Households Connected to National Grid Electn"city by Region by December, 2016*





*Chanzo: REA, 2017*

**Kielelezo Na. 5:** *Percentage Distribution of Houselwlds using Solar Power Electn"city by Region by December, 2016*





*Chanzo: REA, 2017*

**Kielelezo Na. 6:** *Percentage Distribution of Households Connected to Electricity by Source of Energy and Place of Residence by December, 2016*





*Chanzo: REA, 2017*

**Kielelezo Na. 7:** *Percentage Distribution of Households Connected to Electricity by Place of Residence and Main Source of Electricity by December 2016*




*Chanzo: REA, 2017*

***Kielelezo Na. 8:** Exploration Activity Map, National Natural Gas Infrastructure Project and The East Africa Crude Oil Pipeline Project*




*Chanzo:TPDC,2017*

***Kielelezo Na. 9:*** *Hali ya Ugunduzi wa Gesi Asilia Hadi Kufikia Mwezi Februari, 2017*


| **Kitalu cha Ugunduzi** | **Visima vya Uzalishaji/ Ugunduzi** | **Mwaka ilipogundulika** | **Muendeshaji** | **Hali halisi** | **Makadirio ya Ugunduzi (BCF) P90** | **Kiasi Kilichopo (TCF)** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Songosongo | S4, S7,S10 & S11 | 1974 | Panafrican Energy | Imeendelezwa | 880 | 1 – 2.5 |
| Mnazi-bay | MB, MB2,MB3 & MS-x1 | 1982 | M &P | Imeendelezwa | 262 | 3 – 5 |
| Mkuranga | Mkuranga-1 | 2007 | M&P | Haijaendelezwa | | 0.2 |
| Nyuni | Kiliwani-N | 2008 | Ndovu Resource | Imeendelezwa | 0.07 | 0.07 |
| Ruvuma | Ntorya-1 | 2012 | Ndovu Resource | Haijaendelezwa | | 0.178 |
| Ruvu | Mambakofi-1 | 2015 | Dodsal | Haijaendelezwa | | 2.17 |
| **JUMLA YA GESI NCHI KAVU** | | | | | | **4.45 - 10.118** |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Block 1 | Chaza-1 | 2011 | BG Tz | Haijaendelezwa | | 0.47 |
| | Jodari-1 | 2012 | BG Tz | Haijaendelezwa | | 3.53 |
| | Jodari North-1 | 2012 | BG Tz | Haijaendelezwa | | |
| | Jodari South-1 | 2012 | BG Tz | Haijaendelezwa | | |
| | Mzia-1 | 2012 | BG Tz | Haijaendelezwa | | 8.5 |
| | Mzia-2 | 2013 | BG Tz | Haijaendelezwa | | |
| | Mzia- 3 | 2013 | BG Tz | Haijaendelezwa | | |
| | Mkizi -1 | 2013 | BG Tz | Haijaendelezwa | | 0.6 |
| | Taachui-1 | 2014 | BG Tz | Haijaendelezwa | | 1.10 |
| Block 2 | Zafarani-1 | 2012 | Statoil | Haijaendelezwa | | 6.0 |
| | Zafarani-2 | 2012 | Statoil | Haijaendelezwa | | |
| | Lavani-1 | 2012 | Statoil | Haijaendelezwa | | 3.6 |
| | Lavani-2 | 2012 | Statoil | Haijaendelezwa | | 1.4 |
| | Tangawizi-1 | 2013 | Statoil | Haijaendelezwa | | 5.4 |
| | Mronge -1 | 2013 | Statoil | Haijaendelezwa | | 2.5 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Piri-1 | 2014 | Statoil | Haijaendelezwa | | 3.0 |
| | Giligiliani-1 | Aug-14 | Statoil | Haijaendelezwa | | 1.7 |
| | Mdalasini | Mar-15 | Statoil | Haijaendelezwa | | 1.8 |
| Block 3 | Papa-1 | 2012 | BG Tz | Haijaendelezwa | | 2 |
| Block 4 | Chewa-1 | 2010 | BG Tz | Haijaendelezwa | | 1.8 |
| | Pweza-1 | 2010 | BG Tz | Haijaendelezwa | | 1.9 |
| | Ngisi - 1 | 2013 | BG Tz | Haijaendelezwa | | 0.8 |
| | Kamba-1 | 2014 | BG Tz | Haijaendelezwa | | 1.03 |
| JUMLA YA GESI KWA BAHARINI | | | | | | 47.13 |
| | | **JUMLA KUU (TCF)** | | | | 57.25 |


*Chanzo: TPDC, 2017*

**Kielelezo Na. 10:** *Hali ya Ugunduzi wa Gesi Hadi Kufikia Mwezi Februari, 2017*





*Chanzo: TPDC, 2017*

**Kielelezo Na. 11:** *Uzalishaji na Matumizi ya Gesi Asilia kwa Kipindi cha kuanzia Mwaka 2007 hadi 2016*





*Chanzo: TPDC, 2017*

***Kielelezo Na. 12:*** *Mwenendo wa Premium za Uagizaji Mafuta Nchini Mwaka 2016 Kabla ya Cargo by Cargo Tender kuanzishwa*





*Chanzo: PBPA, 2017*

***Kielelezo Na. 13:*** *Mwenendo wa Premium za Uagizaji wa Mafuta ya Petroli Mwaka 2016-2017 baada ya Cargo by Cargo Tender kuanzishwa*





*Chanzo: PBPA, 2017*

***Kielelezo Na. 14:*** *Mwenendo wa Premium za Uagizaji wa Mafuta ya Dizeli Mwaka 2016 - 2017 Baada ya Cargo by Cargo Tender kuanzishwa*




*Chanzo: PBPA, 2017*


***Kielelezo Na. 15:*** *Mwenendo wa Premium za Uagizaji wa Mafuta ya Ndege Mwaka 2016-2017 baada ya Cargo by Cargo Tender kuanzishwa*




*Chanzo: PBPA, 2017*


## B: SEKTA YA MADINI

***Kielelezo Na. 1:*** *Kiasi cha Dhahabu Kilichozalishwa na Kuuzwa Nje na Migodi Mikubwa ya Dhahabu (2007 - 2016)*





*Chanzo: TMAA, 2017*

***Kielelezo Na. 2:*** *Kiasi cha Mrabaha Kilicholipwa na Migodi Mikubwa ya Dhahabu Nchini (2007 - 2016)*





*Chanzo: TMAA, 2017*

***Kielelezo Na. 3:*** *Thamani ya Madini Yaliouzwa Nje na Migodi Mikubwa ya Dhahabu – Madini ya Dhahabu, Fedha na Shaba (2007 - 2016)*





*Chanzo: TMAA, 2017*

***Kielelezo Na. 4:*** *Thamani ya Madini ya Tanzanite yaliyouzwa Nje kwa Mwaka 2011 hadi 2016*





*Chanzo: MEM, 2017*

***Kielelezo Na. 5:*** *Thamani ya Madini ya Almasi yaliyouzwa Nje (2011 – 2016)*





*Chanzo: MEM, 2017*

**Kielelezo Na. 6:** *Uwiano kwa **Asilimia** ya Thamani ya Madini Kulinganisha na Bidhaa Nyingine Zilizosafirishwa Nje ya Nchi (2011 – 2015)*





*Chanzo: MEM, 2017*

***Kielelezo Na. 7:*** *Thamani ya Madini Yaliyosafirishwa Nje ya Nchi (2013 - 2016)*





*Chanzo: MEM, 2017*

***Kielelezo Na. 8:*** *Takwimu za Leseni kuanzia tarehe 01 Julai, 2016 hadi 28 Februari, 2017*





*Chanzo: MEM, 2017*

***Kielelezo Na. 9:*** *Mwendo wa Wastani wa Bei ya Dhahabu katika Soko la Dunia (2007 - 2016)*





*Chanzo: LME/LBMA, 2017*

***Kielelezo Na. 10:*** *Mwendo wa Wastani wa Bei ya Madini ya Fedha katika Soko la Dunia (2007 - 2016)*





*Chanzo: LME/LBMA, 2017*

***Kielelezo Na. 11:*** *Ramani inayoonesha wingi wa madini ya shaba*





*Chanzo: GST, 2017*

***Kielelezo Na. 12:*** *Ramani inayoonesha kiwango cha tindikali (pH value) kwenye udongo Nchini*




*Chanzo: GST, 2017*

***Kielelezo Na. 13:*** *Taarifa za Udahili wa Wanafunzi (2013/14 – 2016/17) katika Chuo cha Madini, Dodoma*




*Chanzo: Chuo cha Madini, 2017*